MBINU SABA:

Ufundishaji wa kusoma na kuandika kwa madarasa ya awali.

Muongozo wa kusoma - Tanzania

http://www.criticalthinkinginternational.org

© CODE, 2016.

YALIYOMO

Mbinu Saba: Ufundishaji wa kusoma na kuandika kwa madarasa ya awali

Muongozo wa kusoma - Tanzania

Viwango na vigezo vya ufundishaji na upimaji

wa ufundishaji wa walimu darasani …….. 6

Mbinu Saba. …….. 8

Mbinu ya kwanza: Kutambulisha ujuzi wa kusoma na kuandika …… 8

Mbinu ya Uzoevu wa Lugha ……. 9

Usomaji wa kushirikiana kitabu ……. 15

Kusoma kwa sauti ……. 19

Mbinu ya Pili: Utambuzi wa kifonolojia ……. 21

Kufundisha utambuzi wa kifonolojia …… 21

Michezo ya kusikiliza kwa ajili ya kukuza utambuzi wa lugha ……. 22

Katika ngazi ya neno . …… 22

Katika Ngazi ya Silabi …… 24

Katika ngazi ya Fonimu ……. 24

Kufundisha Alfabeti …….. 25

Mbinu ya tatu: kuhusisha sauti na herufi (Phonics) …….. 26

Kukusanya maneno kwa ajili ya kujifunza masamiati …… 26

Kunakili maneno kwenye daftari …….. 26

Mazoezi ya maumbo ya maneno ……. 27

Kutafuta maneno …….. 28

Mwendelezo wa maneno ya Kiswahili …….. 28

Mbinu za kufundidhia kuhusisha sauti na herufi (phonics) ……. 29

Ubao wa sauti …… 30

Ubao …… 30

Mbinu ya Nne: Ufasaha katika kusoma ……. 31

Kusoma pamoja ……. 32

Igizo la Usomaji ……. 33

Kusoma kwa jozi ……. 35

Mbinu ya Tano: Ufahamu wa Kusoma …… 36

Hatua katika Utabiri:

Kuwaandaa wanafunzi waweze kujifunza kutokana na kusoma 38

Kupanga kabla ya Kipindi …… 38

Kufundisha msamiati kabla ya somo ……. 38

Mutabiri kutokana na maneno muhimu …… 39

Kufikiri/jozi/Kushirikisha ……. 40

Kuandika/jozi/kushirikisha …… 41

Mwongozo wa utabiri ……. 42

Hatua ya kukuza maarifa:

Kwasaidia wanafunzi wajifunze kutokana na kusoma ……. 43

Zoezi la kusoma kwa kuongozwa: Hadithi ……. 44

Zoezi la kusoma kwa kuongozwa: Kutabiri ……. 45

Kufikiri kwa sauti …… 47

Kuunda taswira akilini …… 48

Kusoma kwa kuongozwa …….. 48

Hatua ya kukazia maarifa: Kutumia maana inayotokana na matini .. 52

Kurudia kusimulia …….. 52

Mpangilio wa hadithi ……. 54

Kutafuta wazo kuu …….. 54

Mchezo wa kuchora …….. 55

Ukweli mara mbili na uongo mara moja …… 57

Kuigiza …….. 58

Kila mmoja anongoza: kuigiza katika madarasa makubwa ….60

Kuuliza maswali ya kutafakari …….. 61

Tofauti za kitaaluma ……. 62

Mstari wa thamani ……. 65

Kuelewa Matini za habari ……. 66

Kujua/kutaka kujua/kujifunza …… 66

Usomaji/ufupishaji katika jozi …… 67

Kufundishana …… 69

Mbinu ya Sita: Msamiati …….. 70

Ramani ya Kisementiki …….. 71

Umbo Mchemraba ……... 72

Mfano - Frayer Model ……. 74

Mbinu ya Saba: Uandishi …….. 75

Uandishi wa pamoja …… 76

Uandishi wa kimawasiliano …….. 77

Vipande Sentensi ……. 78
Mfumo wa Uandishi wa ushawishi …… 81
Fremu ya Shairi …… 81
Warsha ya Uandishi …….. 83

Viwango na Vigezo vya Upimaji wa Ufundishaji wa Walimu Darasani

Kiwango A

Mpango sahihi wa ufundishaji

Andalio la somo lipo na lina mpango halisi wa matumizi ya mbinu za kufundishia kusoma.

Kiwango B

Lugha ya kufundishia

Mwalimu anajali kujenga msamiati, na lugha ya mazungumzo na uwezo wa kusikiliza wa mwanafunzi.

Kiwango Ch

Kufundisha maarifa ya neno, alama, herufi na sauti katika muktadha.

Tafuta ushahidi iwapo mwalimu ana uelewa wa kitu kizima- sehemu-kitu kizima

Kiwango D

Kufundisha usomaji fasaha

Mwalimu anatumia mbinu za RT/CBP kwa usahihi na bila matatizo na kwa kuhusisha maana ya kila wanachosoma

Kiwango E

Kufundisha ufahamu wa kusoma

Mwalimu anajenga ufahamu wa wanafunzi kwa kuhusisha maarifa ya awali na kutumia maarifa haya kwa kuhusisha kila walichojifunza.

Kiwango F

Uteuzi Sahihi na matumizi sahihi ya mbinu

Kiwango G

Kuandika

Wanafunzi wanashiriki katika shughuli za kujifunza zinazohusisha uandishi

Kiwango H

Ushiriki wa wanafunzi na ushirikishwaji

Wanafunzi wanashirikishwa katika utendaji wao kwa wao na pamoja na mwalimu wakati wa somo

Kiwango I

Ufikiri wa wanafunzi

Mwalimu anapanga shughuli za ujifunzaji na uzoefu ambao unkuza uwezo wa juu wa kufikiri

Kiwango J

Upimaji Bainifu

Mwalimu anachukua hatua kupima utayari wa wanafunzi kwa ajili ya kujifunza.

Kiwango K

Ujalivu wa kijinsia

Mwalimu anawajali wasichana na wavulana kwa haki na usawa kwa kuwahamasisha wote kushiriki katika matendo y a kujifunza

Kiwango L

Wanafunzi wote wanajaliwa na kuheshimiwa

Ili kuwepo na ufundishaji mzuri wa kusoma, inabidi walimu wajifunze dhana na mbinu mbalimbali katika maeneo saba yafuatayo:

1. Kuwatambulisha wanafunzi katika ujuzi wa kusoma na kuandika
2. Utambuzi wa kifonolojia
3. Kuhusisha sauti na herufi
4. Ufasaha kaika kusoma
5. Ufahamu
6. Msamiati
7. Kuandika

Ndani ya maeneo haya saba ya kukuza stadi yamo matano ambayo kwa sasa yanasisitizwa na miradi ya LANES na EQUIP-T, hapa yameongezwa mawili. La kwanza, **kuwatambulisha wanafunzi katika ujuzi wa kusoma na kuandika,** ni muhimu kwa sababu wanaojifunza kusoma inabidi waelewe asili na makusudi ya kusoma na kuandika kabla hawajaanza kujifunza stadi hizo. La mwisho, **kuandika,** limejumuishwa si tu kwa sababu kujua kuandika ni sehemu muhimu ya uwezo wa mjuzi wa kusoma, lakini pia kwa sababu kujifunza kuandika humsaidia mwananfunzi kujifunza kusoma.

Mbinu ya kwanza: Kutambulisha ujuzi wa kusoma na kuandika

Kabla ya kufundisha stadi za kusoma na kuandika, inabidi walimu wawafundishe watoto kusoma na kuandika ni kwa ajili ya nini. Kwa nini tunasoma na kuandika? Maandishi ni nini na mpangilio wake katika ukurasa

ukoje? Ni nini haswa kinawakilishwa na maandishi, na kwa namna gani? Baadhi ya dhana hizo kuhusu kusoma na kuandika ambazo ni lazima watoto wajifunze ni hizi zifuatazo:

- Maandishi ni mazungumzo yaliyoandikwa
- Maandishi yameundwa na herufi, zilizoandikwa kwenye vikundi vinavyoitwa maneno, vilivyopangwa kwenye ukurasa kutoka kushoto mpaka kulia na kutoka juu mpaka chini.
- Lugha huja katika sehemu za maneno
- Maneno huweza kuvunjwa kuwa silabi
- Silabi huweza kuvunjwa kuwa sehemu ndogo zaidi zinazoitwa fonimu

Baadhi ya mbinu ambazo walimu wanaweza kutumia kuwafundisha watoto dhana kuhusu kusoma na kuandika ni mbinu ya **Uzoevu wa Lugha**, **Kushirikiana Kusoma Kitabu**, na **kusoma kwa sauti**.

Mbinu ya Uzoevu wa Lugha

Kwa kutumia chaki na ubao, unaweza kufundisha usomaji kwa kutumia njia ya uzoevu wa lugha.

Katika kipindi cha uzoevu wa lugha, mwalimu huwapa hamasa wanafunzi kufikiri na kuongelea kuhusu mada ya kufurahisha. Kila mmoja anahamasishwa kuongea. Baada ya kujadliana kuhusu mada husika kwa kitambo kifupi, wanafunzi wanasoma kwa sauti baadhi ya sentensi kuhusiana na mada husika, na wanafanya mazoezi ya kutamka sentensi hizo mara kadhaa. Halafu wanatamka maneno ya sentensi hizo wakati mwalimu akiziandika ubaoni. Halafu mwalimu anaonyesha baadhi ya maneno huku wanafunzi wakisoma sentensi. Baadaye, mwalimu anachukua baadhi ya maneno kutoka kwenye matini ili wanafunzi waweze kujifunza – si tu kujifunza maeno hayo bali pia kujua namna

yanavyoandikwa, ili waweze kujifunza maneno mengi zaidi yenye kufanana kimuundo.

Somo moja la uzoevu wa lugha linaweza kufundishwa kwa dakika ishirini hadi nusu saa. Kama mada ni ngumu, na/au inafurahisha, inaweza kugawanywa kwa siku tatu au nne.

Zifuatazo ni hatua ambazo unapaswa kuzifuata:

Anza na Kile Kinachosisimua. Zoezi la kujifunza lugha linaanza na mada ya kuvutia ambayo itawahamasisha wanafunzi waweze kuongea. Mada ya kuongelea inaweza kuwa ya kuhusu jambo lolote.

- **Kitu:** Kwa mfano, unaweza kuingia darasani na fuvu la samaki mkubwa ambalo wanafunzi wanaweza kuliona na kuliongelea.
- **Tukio la kufurahisha:** Unaweza kutumia tukio lolote la kufurahisha ambalo limetokea, kama vile mgeni kukaribishwa darasani, au ziara ya mafunzo ya darasa zima, au maonyesho ya kisayansi.
- **Hadithi:** Unaweza kuwasomea wanafunzi nusu ya kwanza ya hadithi na kuwaacha wamalizie kama zoezi la imla.
- **Somo:** Unaweza kujadili kuhusu somo la afya, kama vile njia za kuepuka magonjwa, au njia za kuandaa maji salama ya kuja.
- **Shairi au wimbo:** Unaweza kutumia wimbo au shairi ambalo wanafunzi wanajua tayari, au unaweza kutunga shairi au wimbo mwingine ili waweze kuimba au kukariri.

Kuanzisha Majadiliano. Wape wanafunzi dakika tano za majadiliano kuhusu mada husika. Jitahidi kuwa makini katika matumizi ya maneno ya msingi kuhusiana na mada. Hata kama somo la kuhusu uzoevu wa lugha hulenga kuwa na matamshi ya maneno, unaweza pia kuwafundisha msamiati mpya.

Kuandika Imla. Waambie wanafunzi kuwa utaandika kile wanachosema kuhusu uzoevu wao juu ya mada. Waambie wanafunzi kuhusu matini ambayo wanaelekea kuiandika. Andika kichwa cha matini juu ya ubao kwa maandishi makubwa ili kila mmoja aweze kusoma. Watamke kile neno utakaloandika. Waambie wanafunzi wakusaidie kutaja herufi za maneno: “Herufi ipi natakiwa kuanza nayo kuandika neno hilo?”

Sasa, mwite mwanafunzi azungumze chochote kuhusu mada husika. Jaribu kumsaidia mwanafunzi kusema sentensi yenye maneno matano au sita. Halafu waambie wanafunzi wote wairudie sentensi hiyo walau mara tano hivi.

Kama wanafunzi bado ni wadogo sana, waambie waonyeshe ubaoni sehemu ambayo wangependa uanze kuiandika. Halafu waambie waseme sentensi yenyewe huku ukiendelea kuandika. Kama wanaenda haraka waambie wapunguze kasi ya kuongea. Unatakiwa uwaambie kuwa wasome maneno kadiri unavyoyaandika, ili waweze kuona jinsi yanavyoandikwa.

Halafu mwambie mwanafunzi mwingine naye atunge sentensi. Msaidie aifupishe sentensi hiyo iwe na maneno kati ya matano hadi sita. Halafu, waambie wanafunzi warudie kuitamka hiyo sentensi huku wewe ukiiandika. Endelea kufanya hivyo mpaka ufikishe sentensi nne au tano kwenye ubao.

Soma tena Matini. Kuna hatua tano za kusoma tena matini.

1) Usomaji wa Mwalimu. Kwanza, wewe kama mwalimu soma matini yote huku ukionyesha kila neno. Soma taratibu, lakini kwa uhalisia – kama vile unaongea.

2) Kusoma kwa Pamoja. Halafu waambie wanafunzi wote darasani wasome pamoja na wewe kadiri unavyoonyesha maneno ya kusoma. Jaribu tena kuyasoma kwa matamshi ya kawaida. Rudia hatua hii mara kadhaa.

3) Kurudia usomaji. Sasa soma mstari mmoja huku ukionyesha maneno unayosoma. Halafu rudia tena kuyaonyesha maneno kwenye huo mstari kadiri

wanafunzi wanavyosoma. Rudia kwa kila mstari. Halafu rudia kusoma matini yote.

4) Kusoma kwa makundi. Halafu, unda makundi tofauti ambayo watasoma kwa kupokezana – mwanafunzi mmoja mmoja kila upande, au wanaweza kuwa wasichana peke yao halafu wavulana baadaye nao wanasoma peke yao. Wanafunzi wanaweza kuhitaji msaada – soma nao taratibu.

5) Usomaji wa mtu mmoja peke yake. Hatimaye, unaweza kuwaambia wajitolee mtu mmoja mmoja kusoma. Wanafunzi wanaweza wakahitaji msaada – soma nao taratibu. Msaidie na huyo mmoja anayesoma peke yake ikitokea anahitaji kusaidiwa.

Itunze matini na kuisoma tena baadaye. Ni vizuri sana kuandika zoezi kwenye karatasi kubwa au kadi kubwa kwa kutumia kalamu ya maandishi makubwa, au kipande cha mkaa. Kama huna hivyo vyote, iandike matini yako sehemu moja ya ubao kwa muda wa siku tatu zinazofuata. (Kumbuka kuandika chini yake neno **Usifute!**).

1) Rudia zoezi la kusoma. Tumia mbinu za *usomaji wa mwalimu, kusoma kwa pamoja, kusoma kwa kurudia kilichosomwa, na usomaji wa mtu mmoja peke yake*.

2) Sema sentensi kwa sauti na mwulize mwanafunzi aseme ni sentensi ipi umesoma kadiri unavyozionyesha ubaoni.

3) Sema neno halafu onyesha maneno kadhaa na waulize wanafunzi waseme ni neno gani huku unaonyesha neno husika ubaoni.

Waambie wanafunzi wanakili matini kwenye madaftari yao ya insha. Zunguka na kuona ni kwa namna gani wanaweza kufanya zoezi hili. Unaweza kuwaomba wanafunzi wanaoweza zaidi wawasaidie wenzao wenye uwezo mdogo..

Waambie wanafunzi wasome matini kirafiki. Mwanafunzi mmoja asome mstari mmoja kwa sauti wakati mwingine akisoma kimya. Huyo atakayesoma kimya anaweza kumsaidia mwenzake aliyekwama kusoma. Halafu

wanapokezana, Yule aliyekuwa kimya anasoma kwa sauti halafu mwenzake aliyesoma mwanzo kwa sauti anakuwa kimya huku akimsaidia mwenzake.

“Uvunaji wa Maneno”: Baada ya kusoma matini mara nyingi wanafunzi lazima watunze baadhi ya maneno kwenye kumbukumbu zao vichwani. Sasa unaweza kutaka kujua kama wanafunzi wanaweza kutambua baadhi ya maneno wao wenyewe. Waambie wanafunzi kuwa unataka kuona wanajifunza baadhi ya maeno yaliyomo kwenye matini. Andika kwenye kipande cha karatasi baadhi ya maeno yaliyomo kwenye matini. Waite baadhi ya wanafunzi waje mbele ubaon. Wape neno mojawapo na waambie walitafute neno hilo kwenye matini. Waambie waliandike neno hilo kwenye karatasi yao chini ya neno kama hilo lililomo kwenye matini. Kama watahitaji msaada wa, wasaidie kwa njia ya kusoma sentensi ambayo ndani yake kuna hilo neno. Rudia hatua hii hata kwa maneno mengine.

Ikiwa zoezi hili la kulinganisha maneno ni jepesi kwa wanafunzi, waambie mmoja mmoja kwa muda tofauti kuja mbele ubaoni na kutafuta neno wanalolifahamu. Waambie walionyeshe neno hilo au kuweka kidole kwenye neno husika.Waambie waseme neno hilo linamaanisha nini. Wapongeze ikiwa wamepatia vizuri. Ikiwa wamekosea waambie neno hilo ni lipi, na baada ya hapo onyesha neno walilokuwa wanajaribu kulinganisha nalo. Soma neno hilo na pia waombe wanafunzi walisome pia. Rudia hatua hii kwa maneno mengine ikiwa wanafunzi wamefanikiwa kuelewa. Kama wanafunzi wameweza kunakili matini kwenye madaftari yao ya insha, basi wanaweza kupigia mistari au kuzungushia maneno wanayoyafahamu.

Wanafunzi wanaweza kukumbuka maneno machache tu kutoka kwenye matini za mwanzo. Hilo ni sawa kabisa. Hata hivyo unatakiwa uendelee kuwasomea matini mpya. Kadiri matini zinavyozidi kuwa nyingi, ndivyo na jinsi watakavyoweza kujifunza maneno mengi zaidi. Kurudia kuisoma matini mara kwa mara ndivyo itakavyowasaidia wanafunzi kuendelea kujifunza.

Zoezi la kujaza nafasi katika neno. Funga kipande cha karatasi ngumu cha ukubwa wa neno. Kitumie kipande hicho kufunika neno kwenye mstari wa matini. Waambie wanafunzi kukisia neno. Wasipoweza kukisia, sogeza kadi upande wa kulia ili waweze kuona herufi ya kwanza ya neno, endelea kusogeza kadi kulia hatua kwa hatua mpaka waweze kukisia neno husika.

Futa neno moja au mawili kutoka kila sentensi zilizoko ubaoni. Waambie wanafunzi kuwa yako maneno yamekosekana na waulize kama wanaweza kuyataja hayo maneno yaliyokosekana. Isome matini na wanafunzi. Pumzika kwa muda ukifika mahali ambapo neno linakosekana. Andika maneno yanayokosekana ambayo wanafunzi wanakutajia ili yaweze kujaza nafasi ambako neno lilifutwa.

Kwa wasomaji wasio na uwezo mkubwa, unaweza kuandika maneno yalikosekana chini ya ubao ili uweze kurahisisha zoezi hili.

Tengeza "Ukuta wa Maneno". Ikiwa wanafunzi wengi wanalijua neno, liandike neno hilo kwa maandishi makubwa kwenye kadi au kipande cha karatasi ngumu. Libandike neno hilo darasani kwenye eneo ambalo utaliita "Ukuta wa Maneno ». Ukuta wa maneno unaweza kuwa na maneno 40 kwa wakati mmoja, kwahiyo andaa nafasi darasani kwa ajili ya zoezi hili.

Fanya marejeo ya maneno ya kusoma na rudia kuyasoma maneno yaliyomo kwenye ukuta wa maneno kila siku kwa kuonyesha maneno hayo wakati wanafunzi wakiyasoma. Endelea kuongeza maneno kwenye ukuta wa maneno kila wakati utakapofanya zoezi la uzoevu wa lugha. Kwa kutumia maneno ya kurudiwa rudiwa yaliyomo kwenye ukuta wa maneno itawasaidia wanafunzi kuyakumbuka maneno hayo. Kadiri wanafunzi na mwalimu wanavyopitia maneno yaliyomo kwenye ukuta wa maneno, wanaweza 1) kurudia kusoma

neno wakiyaimba, 2) kurudia kusoma kila herufi wakiimba, na 3) kurudia tena kusoma neno wakiimba.

Unaweza kutumia ukuta wa maneno kuwafundisha wanafunzi kuhusu mpangilio wa herufi za maneno, au kile kinachoitwa mfumo wa sauti za maneno. Tazama sehemu ya “Kujifunza Msamiati” inayofuata kwenye muongozo huu kwa mapendekezo mengi ya jinsi kutumia ukuta wa maneno kwa ajili ya kufundisha mfumo wa sauti ya maneno.

Usomaji wa kushirikiana kitabu

Usomaji wa kushirikiana kitabu hufanyika kukiwa na kitabu kikubwa : kitabu ambacho ni kikubwa kiasi cha wanafunzi wote kuona.

Wakusanye watoto pamoja ili kila mmoja akae karibu kabisa na mwenzake kiasi kwamba wanaweza kuona vizuri kile kilichoandikwa na kujisikia kuwa wao ni jamii moja. Kiweke kitabu katika ubao utakaowasaidia wanafunzi waone vizuri, na mikono yako ipate urahisi wa kuonyesha maneno kadiri unavyosoma. Tumia ufito wa kuonyeshea kila neno unalosoma, na jaribu kuisoma matini hiyo kwa usahihi na kwa ufasaha. Kumbuka, unaposoma ndio unaonyesha mfano ili watoto waige usomaji wako na wajue maana ya usomaji wa ufasaha ni upi.

Anza kwa kutoa maelezo ya jumla kuhusu kitabu, ongelea kile ambacho watoto wanatarajia kukisikia kutoka kwenye kitabu. Kwa mara ya kwanza unaposoma matini, toa utangulizi wa hadithi kwa kutaja kichwa cha hadithi, ukurasa wa mbele, na ukurasa wa taarifa kuhusu kitabu. Kama kuna michoro uliyoandaa basi wape “taswira” kuhusu matini – yaani onyesha michoro iliyopo na unganisha hadithi yako na michoro hiyo.

Halafu soma matini kwa sauti huku ukiwa mwenye kufurahia kadiri unavyopitisha mkono wako kwenye maneno, kifungu kwa kifungu huku

ukisoma. Soma katika hali ya kuigiza vitendo – siyo kwa haraka sana, na si taratibu sana. Wanafunzi na wafuatilie kwa kupitisha macho yao sehemu unazosoma. Itabidi uwe unapumzika nyakati fulani kwa ajili ya kuwauliza wanafunzi watoe maneno ya kutabiri, au kuwauliza wabashiri tukio linalofuata kwenye matini.

Wewe na wanafunzi mnaweza kupokezana kusoma matini husika. Mnaweza kwa pamoja mkasoma ukurasa; yaani, wewe na watoto mnasoma pamoja maneno huku ukionyesha kwa vidole. Unaweza kusoma nao kwa kupokezana; yaani, unasoma kwanza mstari halafu na wanafunzi wanafuatisha ulivyosoma huku ukiyaonyesha maneno hayo.

Unaweza kuwauliza wanafunzi wajibu maswali kuhusu matini husika wakati wa kusoma na baada ya kumaliza kusoma. Haya yanaweza kuwa maswali ya yenye majibu ya wazi. Yanaweza kuhusiana na historia ya mwanafunzi mwenyewe, uzoevu wake, na pengine hata kuhusiana na vitabu vingine ambavyo tayari wameshavisoma.

Ikiwa wanafunzi wameshaiozea matini husika, mwalimu anaweza kuitumia kufundishia hatua muhimu katika kusoma na kuandika.. Mwalimu hatatumia mazoezi yote ya kujifunzia na kitabu kimoja, lakini atachagua yale yanayoendana na kitabu na mahitaji ya watoto.

Kufundisha masomo kwa kutumia Matini

Mwalimu anaweza:-

- kuziba neno kwa mkono au kwa kipande cha karatasi ngumu na kuwauliza wanafunzi kukisia neno kutegemeana na muktadha, au kwa kutumia herufi ya kwanza ya neno, au herufi mbili za mwanzo nk;

- Kuandika sentensi nne au tano kutoka kwenye matini, kwenye vipande vya karatasi na kuwapa wanafunzi waweze kuvipangilia vizuri kadiri ya chati inavyoonyesha;
- kukata sentensi na kumwambia mwanafunzi au wanafunzi waiiweke katika mpangilio sahihi;
- kupitisha kadi za maneno na kuwaambia wanafunzi wazilinganishe na maneno yaliyomo ndani ya matini, au na maneno yanayoanza na herufi zinazofanana nayo, au yale yenye sauti zinazofanana nayo au yale yenye silabi zinazolingana;
- kupitisha kadi zenye herufi ndogo na kuwaambia wanafunzi walinganishe na herufi kubwa kwenye matini, na kinyume chake;
- kuonyesha herufi kubwa mwanzoni mwa maneno na kuelezea kwanini zimeanza mwanzoni mwa maneno;
- kuelezea matumizi ya alama za uandishi;
- kuwaambia wanafunzi kuonyesha maneno ambayo yanaonyesha jinsi kitu kilivyooonekana, au jinsi mtu alivyojisikia, au ambacho mtu alikifanya nk.

Muhtasari wa Maelekezo kuhusu Usomaji wa kushirikiana:

- **Jiandae kwa ajili ya Usomaji wa kushirikiana kitabu.** Chagua kwa makini matini kwa ajili ya kipindi. Matini iwe ni ile ambayo utapenda kuitumia mara kadhaa. Kwa wasomaji wanaoanza kujifunza, matini inaweza kuwa wimbo au ngonjera. Au inaweza kuwa kisasili ambacho kitasimuliwa kwa urahisi. Au kinaweza kuwa na taarifa kuhusu mada yenye mvuto kwa watoto. Andika matini kwa maandishi makubwa kiasi cha kuwawezesha wanafunzi kwenye makundi yao waweze kuyasoma – hii inamaanisha kuwa herufi ziwe walau sentimeta 10 za urefu. Weka na mifano au michoro.
- **Kusoma kwa Mara ya kwanza:**

1. Ipitie matini na wanafunzi. Soma kichwa cha matini na jina la mwandishi. Kama ndo wanaanza, waeleze kuwa kichwa cha habari ndio kichwa cha kitabu. Waeleze kuwa kichwa cha kitabu ndicho kinachotoa picha ya jumla kuhusu kitabu. Waulize ni nini wanafikiri jina hili la kitabu linapendekeza kuhusu mada ya kitabu. Ongezea yale unayofikiri kwa sauti – mawazo yako unayoyatamka kwa sauti ambayo yanaongoza fikra zako.
2. Soma jina la mwandishi, kama lipo. Fafanua kuwa mwandishi ni yule aliyeandika kitabu. Waulize kama wanavijua vitabu vingine vilivyoandikwa na mwandishi. Taja vitabu unavyovijua na waeleze zaidi kuhusu mwandishi.
3. Wajulishe yale wanayoweza kutarajia katika somo – yaani yale wanayotakiwa kutilia maanani.
4. Soma tena kichwa cha kitabu, onyesha jalada na maelezo yake. Waulize wanafunzi wabashiri kitakachotokea ndani ya hadithi, au wanachotegemea kujifunza kutokana na hadithi.
5. Toa utangulizi kuhusu kitabu katika hali ya kutia hamasa. Kama umechora picha sambamba na matini, zionyeshe picha hizo sasa na fanya nao kazi ya kuunganisha hadithi na picha ulizoonyesha.
6. Halafu soma matini katika sauti ya kuigiza. Pitisha mkono wako katika sehemu unazosoma, isiwe kwa haraka sana wala kwa taratibu sana. Jielekeze zaidi kwenye maana ya matini. Waambie wanafunzi washiriki katika kusoma kama wanaweza.
7. Pumzika kidogo kwa ajili ya kuzungumzia matini huku ukisisitiza maana iliyomo. Kumbuka unaposoma wewe ndo unakuwa mfano wa kuigwa na wanafunzi katika usomaji mahiri, na pia kama msomaji anayeweza kutafakari kile anachosoma. Waalike wanafunzi nao watoe maoni yao pia.
8. Pumzika kwa kitambo kwa ajili ya kuwauliza wanafunzi wabashiri kuhusu matini – hasa hasa kabla hujafungua ukurasa mwingine. Kadiri

unavyoendelea kusoma, toa maoni yako kuhusu ubashiri ule unaoonekana kuwa wa kweli.

9. Baada ya kumaliza kusoma waulize wanafunzi hadithi imewapa hisia gani au imewafanya wafikirie nini na kwa nini.

- **Kurudia kusoma matini**

1. Rudia kuisoma matini mara kadhaa, waalike wanafunzi kusoma pamoja na wewe. Waambie warudie kile unachosoma: unasoma mstari wa hadithi na wao wanaurudia. Waambie wasome pamoja na wewe kama darasa, wote mkisoma kwa pamoja.
2. Waambie wapige makofi, waigize sura mbalimbali kuendana na vitendo au visa vya kwenye hadithi. Waalike baadhi ya watoto kuigiza baadhi ya sehemu za hadithi.
3. Iache matini ndani ya darasa ili wanafunzi waendelee kujisomea kwa muda wao. Ikiwezekana tengeza matini ndogo ndogo au sehemu za matini na kuwapa wanafunzi ili waweze kufanya mazoezi ya kusoma wakiwa peke yao. Wanaweza kuzisoma pamoja kwa kupokezana, au kuisoma pamoja katika makundi madogo.

Kusoma kwa sauti

Kusoma kwa sauti kunawakutanisha wanafunzi na lugha ya kwenye vitabu – dhana, msamiati, na muundo wa yaliyomo katika vitabu. Tunapendekeza hatua zifuatazo zitumiwe kila wakati unaposoma kwa sauti na wanafunzi. :

1. **Jiandae kusoma matini** ya kuisoma kwa wanafunzi. Amua unataka isomweje,- kwa utani, maigizo na kwa kuujiuliza maswali ya udadisi. Kama kuna sauti mabalimbali amua jinsi gani unataka kila moja isikike.

Kama unaamua kuacha kusoma ili kuuliza utabiri na majadilidano, amua sehemu gani za kufanya hivyo. Kama kuna maneno au mawazo yasiyofahamika na wanafunzi, hakikisha unayatamka kwa usahihi unayaelezea kwa wanafunzi.

Fanaya mazoezi ya kusoma matini mara nyingi zaidi mpaka uweze kuisoma kwa urahisi, na kwa hisia (angalia kipengele hapa chini kwa mawazo kuhusu kusoma kwa hisia)

2. **Waandae wanafunzi.** Hakikisha wanafunzi wamekaa mahali ambapo wanaweza kukuona na kukusikia vizuri. Kama kuna umuhimu wakumbushe kuhusu tabia ya wasikilizaji wazuri : *mikono kwao wenyewe, macho kwa mwalimu, na masikio kwenye hadithi.* Waambie wanafunzi kichwa cha matini na jina la mwandishi. Mzungumzie kidogo mwandishi kama unafahamu habari zake – mahali alipokulia, na kazi zake nyingine ambazo wanafunzi wanaweza kuzijua.

   Waambie wanafunzi matini inahusu nini, na unafikiri nini kinavutia kwenye matini hiyo

3. **Soma matini kwa hisia**
   Soma taratibu kidogo – kumbuka kuwa wasikilizji wanahitaji muda wa kufikiri na kuelewa unachokisema. Kadiria ukubwa na ukali wa sauti unayotumia. Usikike kama unafurahia unachokisoma.

4. **Fuatilia usomaji**
   Waulize wanafunzi nini wamependa kuhusu matini. Imeawafanya wafikirie nini ? Kwa nini ?

5. **Soma tena matini**

Soma matini kwa mara ya pili. Pumzika usubiri maoni. Kama kuna maneno yoyote yanayorudiwa kwenye kitabu, labda yaandike katika maandishi makubwa kwenye ubao na waulize wanafunzi kuyarudia. Kama kuna mambo ya kuvutia yaliyoibuliwa< tenga muda wa kuyajadili. Kama kuna masuala ya kuvutia, tenga muda kuyapitia na kuyaelewa. Kama kuna maswali ya kuvutia, zungumzia namna ya kuendelea kuyafanyia uchunguzi.

Mbinu ya pili: Utambuzi wa kifonolojia

Lugha huja katika aya, sentensi, na maneno. Maneno yanayosemwa yanaweza kugawanyika katika silabi na vipengele vidogo zaidi viitwavyo fonimu. Kwa mfano, neno **moja** lina silabi : **mo-** na **ja- .** Silabi **mo ,** inaweza kugawanywa zaidi kuwa **/m/** and **/o/ .** Silabi –ja inaweza kugawanywa kuwa **/j/** na **/a/.**

Il kujifunza kusoma, watoto wanahitaji kujua kuwa herufi M inasimama badala ya sauti /m/, herufi O kwa sauti /o/, na kadhalika. Kujifunza kulinganisha herufi na sauti inaitwa *phonics.* Lakini kabla watoto hawajajifunza vizuri kuhusisha sauti na herufi, ni lazima wajifunze kuwa makini na sauti zinazozungumzwa kwenye maneno.

Kufundisha utambuzi wa kifonolojia

Watoto wanaotambua vipande au sehemu za sauti katika lugha wana nafuu hasa kwenye kusoma maneno kwa sababu watagundua sehemu za maneno zinazolingana na herufi. Inabidi walimu wafundishe utambuzi wa kifonolojia katika darasa la chekechea au awali mpaka darasa la pili. Ufundishaji huu unaweza kufanyika katika

kipindi kifupi kila siku – dakika sita au saba. Shughuli za kukuza utambuzi wa kifonolojia zinaweza kufanyika katika viwango kadhaa.

Michezo ya kusikiliza kwa ajili ya kukuza utambuzi wa lugha

Watoto wanahitaji kuwa wasikivu katika lugha – kusikia maneno, kuchezesha miili yao kufuatana na maneno waliyosikia, kupiga makofi kuendeana na mdundo wa lugha, na kutambua viimbo. Vitendo mbalimbali vya kusikiliza vinaweza kuwasaidia kukuza stadi hizi.

Kusikiliza na kubaini maneno maalumu: Katika mchezo huu wa "maneno maalumu" sema neno kwa mfano "barua" na waambie watotokuwa unataka kuwasimulia hadithi ambayo ina neno "barua" na kuwa wao wapige makofi wakisikia neno "barua". Kwa mfano unaweza kusema:

" Mzee Mitimingi anaishi kijiji cha Songambele. Pamoja na umri wake mkubwa mzee huyu hajui kusoma wala kuandika. Siku moja alipata **barua** kutoka kwa mtoto wake anayeishi mjini. Baada ya kufurahia kupata **barua**, Mzee Mitimingi alimwita kijana Keta ili amsomee **barua** hiyo. Keta alikubali na kuifungua **barua** hiyo…"

Unda hadithi kadhaa kwa kutumia neno "barua" halafu waambie watoto wakupe neno maalumu halafu unda hadithi yenye neno hilo. Watoto wanaweza kupokezana kuunda hadithi zao wenyewe zenye "maneno maalumu" ndani yake halafu wasimulie kwa wenzao.

Kisha, unaweza kuongeza kiwango cha ugumu wa maneno maalumu kwa kuwataka watoto wasikilize kubaini maneno mawili pamoja. Maneno hayo yanaweza kuwa kwa mfano: **viazi vitamu** na unaweza kusema:

" Nyumbani kwetu tuna shamba kubwa la viazi. Tumepanda viazi kwenye matuta. Tulipalilia na kumwagilia vizuri hivyo viazi vyetu vilistawi sana. Tumevuna na tunakula na wote tunavipenda sana kwa sababu ni vitamu. Mama ameniambia kuwa kutokana na utamu wake ndiyo maana vinaitwa "viazi vitamu"

Pia watoto wanaweza kusikiliza ili kubaini neno moja lililorudiwa mara mbili kwa mfano: “haraka haraka”

“Maria ni msichana wa darasa la pili. Yeye hupenda kufanya mambo yote kwa haraka. Kila akitembea, akila, akioga, akizungumza yote ni kwa haraka. Siku moja aliitwa na mwalimu naye kwa haraka akaanza kukimbia. Alianguka chini na kuumiza mguu wake, ndipo mwalimu akamwmbia Maria uwe mwangalifu haraka haraka haina baraka.”

Kupiga makofi kwa ajili ya maneno: Unaweza kufanya michezo ya kupiga makofi kwa namna mbali mbali. Wanafunzi kupiga makofi kwa maneno unayotamka ni mchezo rahisi. Kupiga makofi kwa mpangilio maalumu inaleta changamoto zaidi: mikono pamoja, mikono kwenye magoti, mikono kwenye kifua, mikono pembeni ya mapaja. Waambie watoto wapige makofi kufuatana na unavyotamka maneno haya kwa msisitizo:

Watoto-wadogo-wanapoimba-na-kucheza-na-wenzao--hufurahi-sana

Nyimbo, tenzi na mashairi: Nyimbo na tenzi ni njia asili ya kufanya watoto wazingatie sauti, na pia kukariri maneno, vifungu na sentensi ambazo zitasaidia maendeleo ya lugha. Nyimbo, tenzi na mashairi pia huwafurahisha watoto katika wanapojifunza na kurudia rudia.

Mwimbo kama huu ufuatao huwafanya watoto wapige makofi na kufuatilia kwa karibu sana sauti ya wimbo:

Dada nawa nawa

Dada nawa mikono yako

Usishike chakula chako

Mikono ikiwa michafu

Walimu wazoefu wanajua nyimbo nyingi zinazoweza kutumika. Nyimbo za mpito, nyimbo za kutambulisha shughuli Fulani, nyimbo za kusherehekea watu maalum –

zote hizi ni muhimu kwa mwalimu kuwa nazo. Ukimpata mwalimu anaejua nyimbo hizi, ziandike. Na pia ulete kinasa sauti ili uweze kunasa sauti hizi.

Katika ngazi ya silabi

- Watoto wanaweza kupiga makofi kufuata silabi kwenye majina yao – “Ma-ri-a”, “A-i-sha” “Ba-ra-ka”
- Watoto wanaweza kunyanyua mikono wakati mwalimu anasema neno na silabi moja, mbili au tatu
- Wakati mwalimu anasema “silabi moja”, inabidi motto aseme neno la silabi moja; mwalimu akisema ‘silabi mbili’ na anamwita mtoto, huyo motto anasema neno la silabi mbili na kuendelea.

Katika ngazi ya Mizani (sauti zinazofanana):

- Watoto hutakiwa kutoa maneno yanye sauti za mwisho zinazofanana ili kumalizia nyimbo:
  Moja, moja, moja
  Mtoto ana _____ (ngoja)
  Mbili, mbili, mbili
  Napenda _____(pilipili)

- Mwalimu anaposema neno kusudiwa kama vile *mbili* watoto wananyosha mikono wakisikia neno linaloendana nalo kwa sauti kati ya maneno anayosema mwalimu kama: *filimbi, pilipili.*
- Mwalimu anaposema neno kama *kaa* halafu anatamka sauti /p/, watoto wanasema neno jipya linaloanza na sauti /p/ na linaloendana na *kaa: paa.*

Katika ngazi ya fonimu

Kuna aina tatu za mazoezi ambazo hutumika kuongeza utambuzi wa fonimu kwa watoto. Moja ni **kutenganisha fonimu.** Kutenganisha ina maana kuvunja kitu ili kupata sehemu ndogo ndogo. Zoezi la kutenganisha sehemu linawataka watoto wachukue maneno yaliyosemwa na kuyavunja kuwa sauti moja moja.

- Zoezi la kuzungumza huwa hivi: “Nikisema paka /p/ /a/ /k/ /a/, ninyi mnasema **dada, kata, na kaka** kwa namna hiyo hiyo.

Njia ya pili ya watoto kutambua fonimu ni kuchnaganya fonimu katika maneno. Kwa mfano:

- Mwalimu anauliza, “Neno gani ninapata nikiongeza sauti “a” “sah” “lih” au “dhah” “hah” “bh”

Njia ya tatu ya watoto kutambua fonimu ni kuondoa kabisa fonimu kutoka kwenye neno na kusema neno gani limebaki. Kwa mfano:

- Mwalimu anauliza, “ Neno gani linapatikana nilkiliondoa sauti “kah” kutoka “taka” ? au kama nikondoa sauti “gah” kutoka “panga”?

Mazoezi ya fonimu yanaweza kuwa yakimchezo na ya kufurahisha kwa mfano,watoto wanaweza kuimba wimbo wenye maneno badala ya sauti za irabu.: (Mwalimu aandae wimbo ambao anaweza kubadili irabu zilizo ndani ya maneno.

Kufundisha Alfabeti

Kutumia Majina: Walimu wananweza kuvuta usikivu wa watoto kwenye alfabeti kwa kuzingatia majina. Mwalimu anaandika jina la kila motto kwenye kipande cha mbao na aweke majina yote kwenye boksi. Kila siku mwalimu anatoa jina moja na kumwita motto huyo mbele ya darasa na kumuuliza maswali kuhusu vitu anavyopenda. Kisha mwalimu anaweka jina la motto kwenye ubao wa matangazo na kueleza kuwa neno hili ni jina. Mwalimu anaweza kuonyesha herufi, huku akisoma kutoka kushoto kwenda kulia na kuwataka watoto wahesabu herufi. Mwalimu anaweza kweka msisitizo kwenye herufi ya kwanza katika jina hilo. Kama jina ni Mariamu, mwalimu anaweza kuwauliza kama wanafunzi wanaweza kubaini herufi ndogo inayofanana na herufi kubwa ya kwanza katika jina Mariamu.Malimu anaweza kuuliza kama wanafunzi wengine wana herufi M ya kwenye jina Mariamu, katika majina yao (kila mtoto jina lake limeandikwa kwenye dawati lake). Kwa kuwa kitendo hiki hufanyika siku baada ya siku, watoto wanataja herufi zaidi na zaidi pamoja na herufi nyingine zinazounda kila jina, herufi zote kubwa na ndogo.

Herufi zinazoruka: Nadharia ya Ufundishaji wa utendaji ya mwandishi Patricia Cunningham (Cunnigham na Allington, 2003), inaleta wazo linalohusishaherufi na sauti katika akili za watoto. Mwalimu (au mwalimu na darasa), hufikiria mwendo au kitendo ambacho kinaweza kuainishwa na kila herufi ya alfabeti. Kisha watoto hutaja herufi kwa sauti na kufanya vitendo: RUKA kwa R, KAA kwa K, IMBA, kwa I na

kadhalika. Darasa linaweza kwenda nje kwenye uwanja ili kufanya mazoezi kwanza, kuwasisimua, na baadae herufi wanaweza kufanya vitendo kwa kufuata herufi wakiwa darasani. Itafurahisha zaidi mwalimu akiita herufi na kuwataka wanafunzi kufanya kitendo, au kuonyesha kitendo na kuwataka wanafunzi kutamka herufi hiyo.

Mbinu ya tatu: kuhusisha sauti na herufi (Phonics)

Ikiwa unatumia njia ya uzoevu wa lugha, kusoma kwa kuongozwa, au njia nyingine ya kufundishia kusoma, unatakiwa utenge sehemu ya muda kila siku kuwaonyesha wanafunzi namna ya kusoma maneno.

Katika sehemu hii tutaonyesha njia kadhaa za kufuata kwa ajili ya kuwaongoza wanafunzi namna ya kujifunza maneno na maumbo ya yake. Njia kuu ni ya kutumia ukuta wa maneno. Kwa njia hii ya ukuta wa maneno, unaweza kutumia njia ya kupangilia maneno. Tutaona pia njia ya kutafuta maneno kama mojawapo ya njia ya kujizoeza mifumo ambayo wanafunzi wanajifunza kwa njia ya kuchambua maneno. Mbao za sauti, na kuunda na kubomoa maneno ni njia nyingine zinazoweza kutumika kuwafundisha wanafunzi juu ya mfumo wa maneno.

Kukusanya Maneno kwa ajili ya Kujifunza Msamiati

Ni vizuri sana endapo wanafunzi watajifunza maana za maneno ambayo walau wameshakutana nayo katika usomaji. Kuna njia mbalimbali za kukusanya maneno kwa ajili ya kuongeza msamiati wa lugha.

Njia ya uzoevu wa lugha: Endapo kutakuwa na maneno 20 katika ukuta wa maneno, itabidi uanze kujifunza kwa kuangalia mfumo wa maumbo yake. Utafanya hivyo kwa kutaja sifa mojawapo na kuwaambia wanafunzi wataje

maneno yote yenye sifa uliyotaja (kwa mfano, yale yanayoanza na herufi inayofanana, au yenye irabu za kufanana nk). Andika kila neno linalotajwa na wanafunzi. Halafu bandika maneno yote yenye sifa hiyo katika safu kwenye ukuta wa maneno.

Kunakili Maneno kwenye madaftari

Ukishaanza kuandika maneno kwenye ukuta wa maneno, maneno mengine yanaweza kuendelea kuongezwa. Maneno haya yanatokana na vipindi vingine vya uzoevu wa lugha, au kutokana na mazoezi ya kusoma au kuandika ambayo wanafunzi wanafanya.

Baada ya kufundisha mfumo wa muundo wa maneno, waambie wanafunzi kunakili maneno hayo kwenye madaftari yao ya insha. Hakikisha kuwa maneno hayo kwenye ukuta wa maneno yanasomwa kila siku kwa njia ya kuimba.

Mazoezi ya Kujifunza Maumbo ya Maneno

Mbali ya kukusanya maneno yanayofanana katika muundo wa herufi, unatakiwa pia kuonyesha jinsi muunganiko wa silabi kwa namna mbalimbali unavyoweza kuunda maneno mapya. Kwa mfano, kama ukiandikaubaoni sentensi: **Pili ana maji,** unaweza kuweka mikono yako kwenye neno maji, naulisome pamoja na watoto. Kisha liandike neno peke yake halafu waambie watoto wasome tena, huku wakipiga makofi wanapotaja kila silabi. Kisha andika silabi **ma-** na **ji-** kila noja peke yake. Sasa weka mikono yako kwenye neno **ana** na watake watoto walisome tena huku wakipiga makofi wanapotaja kila silabi. Kisha andika silabi **a-** na **–na** zenyewe. Waambie watoto watafute silabi katika **ma-, -ji, a-,**na **-na** ambazo zinaweza kuungwa na kufanya neno jipya (**jina,** n.k.)

Kutafuta Maneno

Baada ya wanafunzi kujifunza kundi la maneno yenye maumbo fulani, unaweza kuwapeleka katika hatua ya kutafuta maneno.

Kwanza, wanaambiwa waangalie maneno ambayo tayari wameshajifunza. Maneno hayo yaandikwe kwenye ukuta wa maneno. Watayaangalia katika chati ya kujifunzia lugha, na wanaweza kuyaangalia kwenye kitabu wanachosoma, au wanayaangalia kwenye matini (yenye maandishi makubwa) iliyobandikwa kwenye kuta za darasani.

Wanafunzi wanaweza kuyatafuta maneno ambayo yanafanana kimaumbo na yale ambayo tayari wamejifunza. Kadiri maneno hayo yanavyopatikana, yanaandikwa kwenye ukuta wa maneno.

Mwendelezo wa maneno ya Kiswahili

Mwendelezo wa maneno huwa katika ngazi mbalimbali:

Herufi-kwa-fonimu: Herufi huendeleza sauti ndogo za matamshi zinazoitwa fonimu na kwenye Kiswahili tofauti na Kiingereza, herufi huwa sambamba na fonimu. Baadhi ya herufi huendeleza sauti za irabu – **a, e, I, o, na u** na baadhi huendeleza sauti za konsonanti – **b, l, w, s,** na nyingine.

Wakati mwingine irabu mbili zinaweza kuendelezwa moja baada ya nyingine kama vile katika **s<u>aa</u>, ch<u>oo</u> (***dhau)*

Wakati mwingine konsonanti zinatamkwa haraka moja baada ya nyingine, kama vile **bw** kwenye **<u>bw</u>ana** na **kw <u>kw</u>isha.** Hizi huitwa **konsonanti ambatano.** Ukitamka maneno taratibu utasikia kila sauti ya konsonanti.

Baadhi ya sauti za konsonantihuendelezwa na herufi mbili, kama vile **ch** kwenye **chai** na **dh** kwenye **dhau.** Kumbuka kuwa hata kama unatamka maneno hayo taratibu kiasi gani, hauwezi kutamka sauti za herufi mbili za konsonanti kwa kuzitenganisha, herufi hizo mbili kwa pamoja huendeleza fonimu moja.

Herufi kwa silabi: Kulinganisha na Kiingereza, Kiswahili kinasilabi chache zaidi ambazo huunganishwa kwa namna mbalimbali kupata maneno tofauti. Silabi kama vile **ki-, na-, mwa,** na nyingine huweza kutoa maneno mengi.

Silabi rahisi: Silabi rahisi hujumuisha konsonanti moja na irabu moja. Walimu wamekuwa wakiwafundisha watoto kusoma silabi kutumia konsonanti moja na irabu tofauti. Kama: **ba, be, bi, bo, bu** na **ma, me, mi, mo, mu.**

Silabi chngamano: Silabi changamano huundwa na muunganiko wa konsonanti na irabu zaidi ya moja. Baadhi huusisha konsonanti changamano kama vile **cha** na **dha.** Zingine huusisha konsonanti ambatano, kama vile **mwa, ndi, ngo,** na **mbe.**

Silabi ambazo ni mofimu za kisarufi: Baadhi ya silabi ni mofimu – yaani, vipengele amabvyo hubadilisha maana ya neno. Kwa mfano **u-** kwenye **uhuru, pa-** kwenye **pamoja, hu-** kwenye **hujui** na **ni-** na **li-** kwenye **nilipenda.** Changamoto ya silabi za mofimu si tu kutambua na kuzitamka, lakini pia kuelewa athari zake kwenye maana za maneno.

Mbinu za kufundisha uhusishaji wa sauti na herufi

Ubao wa sauti: Ubao wa sauti ni kifaa cha kuwaonyesha wanafunzi jinsi maneno yanavyoundwa. Kata kipande kikubwa cha bango yenye umbo la mstatili kasha bandika mikanda mitatu ya rangi tofauti kutoka kwenye bango ukikatiza upande mrefu wa bango. Sasa tengeneza kadi za grafimu ambazo ni kubwa kiasi cha kutosha kwa wanafunzi kusoma, lakini ndogo kuweza kutosha katika nafasi zilizotokana na kubadika mkanda kwenye bango. Zigeuze ili upande wa urefu uwe juu, andika herufi

ya ukubwa wa kutosha katika sehemu ya nusu ya juu tukwa kila kadi (sehemu ya chini ya kadi itafunikwa kwenye mfuko). Andaa kadizenye konsonanti na zingine zenye irabu.

Kadi za konsonanti zitakuwa na herufi: **b, c, d, f, g, h, j, k, l, m, n, p, r, s, t, v, w,** na **z.** Kadi za konsonanti changamano (herufi mbili zinazotoa sauti moja) ziwe n ach**, th, sh, ng, ch,** na **dh.**

Kadi za irabu ziwe na **a, e, I, o,** na **u**.

Mfuko wa juu ni kwa ajili ya kuhifadhi konsonanti ambazo wameshajifunza na mfuko wa kati kwa ajili ya irabu ambazo wameshajifunza. Mfuko wa chini ni kwa ajili ya kuunda maneno. Bahasha ya manila inaambatanishwa kwa nyumaya bango la sauti kwa ajili ya kuhifadhikadi za grafimu.

Kutumia bango la sauti, weka konsonanti ndani ya mfuko wa chini. Tamka sauti yake, kasha weka irabuupande wake wa kulia na utamke sauti yake. Sema sauti zote na kisha tamka silabi. Sasa waambie wanafunzi wasome silabi.. Ondoa konsonanti na waambie wanafunziwasome silabi. Endelea kwa kwa kubadili konsonanti kwa irabu na kuwataka wanafunzi wasome matokeo.

Ubao: Hatua hizi zinaweza pia kufanyika katika ubao, kwa kuandika safu ya irabu, safu ya konsonanti, na silabi – na kwa kubadilisha konsonanti na silabi moja halafu nyingine kuunda silabi mpya.

Utaratibu huu unaweza kuendelezwa katika silabi, kuziunganisha kupata maneno.

Kumbuka kila wakati kutumia njia ya kufundishia ya nzima- sehemu- nzima unaposhughulikia uhusishaji wa sauti na herufi.

1. **Nzima**: Anza kwa kusoma sentensi nzima yenye maana
2. **Sehemu:** Jifunze dhana katika uhusishaji wa sauti na herufi

3. **Nzima:** Soma tena sentensi zenye maana ambazo zina maneno uliyojifunza

Mbinu ya nne: Ufasaha katika kusoma

Ili mtu aweze kuwa mahiri katika kipaji chake hana budi kufanya mazoezi mengi. Ili wanafunzi wawe mahiri katika usomaji wanahitajika kufanya mazoezi mengi ya kusoma tena na tena. Lakini kuna mtego: mbebaji vitu vizito haiwezi kunyanyua vitu vizito kushinda uwezo wake. Na wanafunzi hali kadhalika, wataweza kufanikiwa katika kuelewa wanavyosoma iwapo tu matini na makala ni zile wanazoweza kusoma.

Katika sehemu hii tunaangalia njia mbalimbali za kuwasaidia wananfunzi waweze kuwa wasomaji wazuri – yaani kusoma sentensi kwa urahisi, kwa kasi nzuri na kwa kuelewa wanachosoma.

Njia ya kwanza na ya pili, Kusoma kwa Pamoja na Kusoma Wawili wawili, zinaweza kufanyika kwa kutumia matini ambazo zinatumika kwenye zoezi la uzoevu wa lugha, au kwa vitabu vilivyoandikwa kulingana na kiwango chao cha usomaji. Njia ya tatu, Ukumbi wa Wasomaji, huwa na ufanisi endapo zitatumika habari kutoka kwenye matini na hadithi ambazowanafunzi wanaweza kusoma kwa urahisi, au ambazo zina ugumu kidogo zaidi ya kiwango chao.

Kusoma kwa Pamoja

Kusoma kwa pamoja kunaweza kutumika kwa kusoma aya au shairi lililoandikwa ubaoni, au kwenye vitabu ambavyo wanafunzi wanavyo. Kusoma kwa Pamoja kunaweza pia kufanyika kwa matini zile ambazo mwalimu ameziandaa na kaziandika ubaoni. Matini hizo zinaweza kuwafundisha wanafunzi kuhusu sayansi, maarifa ya jamii, au afya. Au zaweza pia kuwa mashairi yenye vichekesho, vina, mizani, na kufurahisha – matini nzuri kwa ajili ya mazoezi ya kusoma kwa kuitikia kwa sauti .

> Kusoma kwa Pamoja ni njia muhimu sana kwa sababu kuu tatu:
> *1) inawapa wanafunzi nafasi ya kufanya mazoezi ya kusoma ili waweze kuwa na uwezo wa kusoma kwa kujiamini na kwa ufasaha – yaani wanaweza kuunganisha mambo kwenye matini kwa urahisi zaidi.*
> *2) inawasaidia kuyazoea maneno na kuweza kuyatambua kwa haraka.*
> *3) inawapa wanafunzi njia ya kutafsiri matini na kuonyesha uelewa wao kwa njia ya sauti zao.*

Siri iliyofichika ya “Kusoma kwa Pamoja” ni kumfanya kila mwanafunzi asome matini mara kadhaa kwa kuifurahia. Hii ni nzuri kwasababu zoezi la kusoma matini litamfanya mwanafunzi asome kwa ufasaha zaidi.

Kusoma kwa Pamoja hufanywa kwa kufuata hatua zifuatazo:

1) Chagua vipande vya matini kwa ajili ya kusomwa – mistari kadhaa kwa kila kipande.
2) Ligawe darasa katika makundi mbalimbali (inaweza kuwa upande wa kushoto, kulia; wasichana, wavulana; nk.).
3) Ita kila kundi kusoma kipande chake, kila kikundi kwa mara moja.
4) Waambie wasome matini kwa namna tofauti: kwa sauti kubwa, ndogo; taratibu sana, haraka sana nk..

5) Waambie wasome matini kama wahusika wa aina tofauti: mtu shujaa, mtu mwoga, mwenye usingizi, mpole, mwenye furaha nk.
6) Kama matini inafaa, basi andaa makundi yaweze kusoma kwa majadiliano – kundi moja linasoma kwanza, halafu jingine linajibu.
7) Kumbuka kuwa ni muhimu kuwafanya wanafunzi wasome mara nyingi – kufanya mazoezi ni muhimu kwao.

Igizo la usomaji

Igizo la usomaji linatilia mkazo ufasaha, mantiki na uigizaji. Wanafunzi wanafanya mazoezi ya kusoma matini kwa sauti, na kutumia sauti zao kuigiza maana mbalimbali zilizomo kwenye matini. Igizo la usomaji ni zaidi ya kufanya michezo ya kuigiza jukwaani, isipokuwa tu badala ya kukariri mistari ya maneno, wanafunzi wanasoma moja kwa moja kwenye matini.

Huku wakijiandaa kusoma matini ya kutungwa kwenye igizo la usomaji, wahusika lazima wajadili kuhusu muundo wa matini, wahusika, na sifa za wahusika hao. Halafu watatakiwa kusoma sehemu za matini hiyo mara kadhaa ili waweze kuzisoma kwa ufasaha kwa mitindo tofauti waliyopanga kuitumia.

Inasaidia ikiwa mwalimu anayefundisha atawauliza wanafunzi,

- “Mhusika wako anajisikiaje sasa? Unatoa sauti gani ukijisikia katika hiyo? Je, sauti yako inabidi iwe ndogo au kubwa? Unatakiwa kuongea haraka au taratibu?”

- “Je, mhusika wako atajisikiaje akisikia kile ambacho mwenzake anasema? Je, mhusika wako atatoa sauti gani baadaye?”

- “Kitu gani kinaendelea sasa katika hadithi hii? Je, mhusika wako anaamuaje kuhusu hilo?”

- “Je, mhusika wako anabadilikaje kadiri visa vinavyobadilika kwenye hadithi?”

Wape wanafunzi nafasi wasome matini mara nyingi zaidi ili kupata mazoezi mazoezi. Simama na wafundishe ikitokea kuna sehemu hawasomi kwa ufasaha au kwa kutoigiza vizuri matukio. (Kumbuka kuwa kusoma sentensi moja mara kwa mara inasaidia kuwafanya wanafunzi wakuze uwezo wa kusoma kwa ufasaha). Mwalimu na wanafunzi wengine wanaweza kutoa maoni na mapendekezo baada ya zoezi la kusoma. Hatimaye, mtatakiwa kufanya maigizo ya matini mara nyingi iwezekanavyo, hasa mbele ya hadhira.

Hizi ni hatua za kufuata kwa ajili ya igizo la somaji.

1. Andika matini kwenye ubao kwa ajili ya igizo la usomaji. Acha maneno ambayo hayahitaji kusomwa kama vile “alisema”, “alijibu”, au “walipiga yowe”.
2. Igawe matini katika sehemu kadhaa zenye sentensi moja au mbili. Kunaweza kuwa na sehemu hadi ishirini.
3. Weka alama sehemu zile zitakazosomwa na wasomaji tofauti. Tumia alama kama vile **herufi kubwa** kuwakilisha jina la kila mhusika, na herufi kubwa **M** ikifuatiwa na **namba ya msimulaji 1, 2, 3,** nk.
4. Kama utataka darasa zima wasome matini kwa wakati mmoja, basi toa kila sehemu kwa wanafunzi kadhaa (kwa mfano, wanafunzi watano watasoma pamoja wajibu wa mhusika mkuu, na watano wengine watasoma taarifa za mhusika mwingine nk). Au unaweza kuwa na kundi la wanafunzi ishirini kwa mara moja ambao watapokezana kusoma matini kwa wenzao darasani.
5. Jaribu kuzifanya sehemu nyingine kuwa nyepesi kusomeka kuliko nyingine. Zile sehemu nyepesi wape wale ambao uwezo wao ni mdogo na zile ngumu wape wale wenye uwezo mkubwa.

Kusoma kwa Jozi

Kusoma kwa jozi ni njia nzuri ya kuitumia ikiwa jozi za wanafunzi au kundi dogo la wanafunzi wanatumia kitabu kimoja. Usomaji wa wawili wawili huwawezesha wanafunzi wengi kusoma kwa wakati mmoja; wakiongozwa na mwenzao.

Katika usomaji wa jozi wanafunzi wanaweza:-

- Kupokezana kusoma sentensi au kurasa
- Kusaidiana kuelewa maneno mageni
- Kuulizana maswali baada ya kuachiana nafasi ya kusoma

Kusoma kwa jozi kunaweza kufanyika kwa kutumia matini iliyosomwa kwa imla au kitabu kilichandikwa kulingana na ngazi ya usomaji wa wanafunzi. Ni muhimu matini husika iwe ya kiasi ambacho wanafunzi wanaweza kusoma bila makosa mengi.

Wakati wa kusoma kwa jozi:-

1) Tafuta matini ambayo wanafunzi wataweza kuisoma yenye ugumu kiasi.
2) Amua kuhusu ukubwa wa sehemu ya kusoma – kama ni aya au kurasa.
3) Wapange wanafunzi katika jozi, au waweke wanafunzi katika makundi ambayo itakuwa rahisi kwao kushirikiana kusoma matini moja.
4) Waambie wapokezane kusoma. Waambie kiwango cha kila mmoja anachotakiwa kusoma.
5) Waambie wale ambao hawasomi wasikilize kwa umakini na kuwa tayari kutoa msaada kwa wenzao wanaopata shida wakati wa kusoma maneno magumu.

6) (Siyo lazima) Waambie wanafunzi wanaosikiliza waulize maswali mawili au matatu baada ya wenzao kumaliza kusoma.

Mbinu ya tano: Ufahamu

Katika sehemu hii utapata mapendekezo ya jumla ya kuwawezesha wanafunzi kukuza ufahamu. Kumbuka kuwa mapendekezo yaliyo mengi yanaweza kutumika pia wakati mwalimu anawasomea wanafunzi matini kwa sauti.

Kipindi chenye ufanisi kina vipengele vitatu: ***maandalizi*** ni hatua ya kutoa utangulizi wa mada na kujenga hamasa kwa wanafunzi; ***kuunda maarifa*** ni hatua ya kutoa taarifa mpya au ujuzi kwa wanafunzi; na ***kukazia maarifa*** ni hatua ambayo wanafunzi wanatafakari na/au wanatumia maarifa ya kile walichojifunza. Zifuatazo ni mbinu zinazotumika kwenye somo hili ambazo ni za muhimu sana.

Mbinu zinazotumika katika hatua ya maandalizi

- Kupanga kabla ya kipindi
- Kufundisha msamiati kabla ya somo
- Kutabiri kutokana maneno ya msingi
- Kufikiri/Kuwa katika jozi/Kushirikishana
- Kuandika/ Kuwa katika jozi/Kushirikiana
- Mwongozo wa utabiri

Mbinu zinazotumika katika hatua ya kukuza maarifa

- Zoezi la Usomaji kwa kuongozwa
- Zoezi la Kusoma – Kufikiri kwa kuongozwa

Mbinu zinazotumika katika hatua ya kukazia maarifa

- Kurudia kusimulia matini

- Mwongozo wa hadithi
- Kutafuta wazo kuu
- “Mchezo wa Kuchora”
- Ukweli mara mbili na uwongo
- Kuigiza
- Kila mmoja anaongoza: Kuigiza kwenye darasa kubwa
- Kuuliza “Maswali ya kufikiri”
- Utata katika taaluma
- Mstari wa Msimamo/thamani

Tafadhali kumbuka kuwa kama muda wa darasani ni mfupi, njia ya kufaa ni kuhakikisha hizo hatua tatu zote zinafanyika ndani ya vipindi viwili vya darasani. Jambo la muhimu ni kwa wanafunzi kuwa na muda wa kutafakari na kuongelea kuhusu yale wanayosoma.

Ufahamu unahitaji mbinu mballimbali wakati wanafunzi wanasoma matini za habari badala ya zile za simulizi. Katika sehemu ya mwisho ya sehemu hii kuna njia tatu za kuelewa matini za kuhabarisha: **Kujua/kutaka kujua/Kujifunza, Kusoma kwa jozi/kufupisha kwa jozi,** na **Kufundishana**

HATUA KATIKA UTABIRI: KUWAANDAA WANAFUNZI WAWEZE KUJIFUNZA KUTOKANA NA KUSOMA

Mbinu nzuri za hatua ya utabiri ni kupanga kabla ya kipindi, kufundisha msamiati kabla ya somo, kutabiri maneno ya msingi, kufikiri/kuwa katika jozi/kushirikishana, na kuandika/kuwa katika jozi/kushirikishana.

Kupanga kabla ya Kipindi

Kama wanafunzi wanajua kidogo sana kuhusu mada, inabidi uwape maelekezo ya awali. Ndani ya dakika chache tunaweza kuwapa wanafunzi mawazo ya msingi ambayo yatawasaidia kuelewa mada husika ya kusomwa kwa sauti. Wape maelezo mafupi kuhusu mada itakayosomwa kwa sauti. Waambie baadhi ya mambo ambayo watajifunza kutokana na kusikiliza matini ikisomwa kwa sauti.

Kufundisha Msamiati kabla ya somo

Matini huwa na istilahi mpya ambazo wanafunzi hawajawahi kuzisikia na baadhi ya taarifa ambazo hawazijui. Hivyo, mwalimu atahitaji kufundisha kabla istilahi ambazo wanafunzi watakuwa hawazijui.

Hatua za kutafuta msamiati kabla ya kipindi ziko wazi:

1. Kwanza pitia matini na onyesha kila neno ambalo unajua wanafunzi watakuwa hawalijui. Tafuta maneno matano au sita kati ya hayo halafu yaeleze maana yake kabla hujaanza kufundisha.
2. Kwa kila istilahi, amua kuhusu
    a) maana iliyo nyepesi zaidi ambayo wanafunzi wataelewa
    b) mfano wa matumizi ya istilahi hiyo kwenye sentensi ambao itasaidia neno husika kueleweka zaidi
    c) ikiwezekana basi iwepo picha au mfano halisi wa kitu kinachomaanishwa ili kionyeshwe
    d) swali kwa wanafunzi ili kuwasaidia waweze kutafakari zaidi kuhusu istilahi hiyo.
3. Halafu fundisha kila istilahi kabla hujaanza kusoma au kabla hawajaanza kusoma.
4. Wakati wa kusoma, unaweza kuwakumbusha kuhusu istilahi hiyo wakikutana nayo kwenye matini.

5. Unaweza kuongeza maneno hayo kwenye ukuta wa maneno na yapitie tena baadaye pamoja na wanafunzi.

Kutabiri kutokana na Maneno Muhimu

Kutabiri Kutokana na Maneno Muhimu inamaanisha mkakati wa kutumia msamiati na ubashiri katika kuangalia maneno yale yanayoleta picha nzima ya hadithi husika na kabla wanafunzi hawajaisikia au kuisoma, inawafanya watumie mawazo yao kuunda hadithi kwa kutumia maneno yote yaliyochaguliwa. Ni njia nzuri sana ya kuibua udadisi kuhusu hadithi, na kuhimiza usikivu makini.

Hatua hizo ni:

1. Mwalimu anachagua kwa makini maneno kati ya 5 na 6 kutoka kwenye hadithi ambayo wanafunzi watakuwa wakisikiliza au kusoma wakati wa kipindi. Haya lazima yawe ni maneno yatakayoonyesha dhana muhimu, vitu, vitendo, au hisia ambavyo vina mchango muhimu katika hadithi.
2. Mwalimu anaandika maneno haya kwa maandishi makubwa ubaoni na kuyafunika mpaka wakati wa kutumia mbinu hii ukifika.
3. Wakati wa kuanza kipindi ukifika, mwalimu anaonyesha hayo maneno na kueleza kuwa yametoka kwenye hadithi watakayosikiliza/kuisoma. Mwalimu anataja na kueleza aina ya hadithi watakayosikiliza (kwa mfano, inaweza ngano, kisasili, tukio la kishujaa, uandishi wa kubuni nk).
4. Huku mwalimu akionyesha kila neno, taratibu atayasoma kwa sauti na kuwaomba wanafunzi kurudia kusoma. Ikibidi, mwalimu anafafanua maana ya maneno, au kuwaomba wanafunzi waeleze maana yake.
5. Baadaye mwalimu awauliza wanafunzi, ama mmoja mmoja au wakiwa wawili, kwa haraka watengeneze hadithi fupi zikiwa na hayo maneno yote.
6. Kwakuwa inalengwa kuwa hilo liwe ni zoezi fupi, si muhimu sana kwa wanafunzi kuandika hadithi zao. Wanaweza kuhimizwa

kuandika sentensi na maneno ili yawasaidie kukumbuka wakati wa kushirikishana hadithi na wenzao darasani. .

7. Baada ya dakika chache, waalike wanafunzi kuwasimulia wenzao hadithi zao, au ikiwa wametunga hadithi wakiwa wawili, basi wawashirikishe wenzao wa jozi nyingine hadithi yao.
8. Kama muda utaruhusu, mwalimu anaweza kumchagua mwanafunzi mmoja au wawili kusimulia hadithi yao darasani. Mwalimu itabidi azipokee hadithi kama njia ya kuwapa moyo pasipo kusema kama zinafanana au hazifanani na ile watakayosikia au kusoma darasani.
9. Baada ya kusomeana hadithi darasani, mwalimu anaanza kwa kusimulia au kusoma hadithi ambayo ina maneno hayo. Wanafunzi wahimizwe kuyasikiliza maneno yanayojitokeza, na kuona kama hadithi zao zinafanana na inayosimuliwa au kusomwa, au ziko tofauti. Baada ya kusoma, wale waliotunga hadithi pamoja wanaweza kujadiliana na wenzao na kulinganisha hadithi zao na ile iliyosomwa.
10. Maneno yaliyojitokeza yanaweza kuongezwa kwenye ukuta wa maneno kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

Kutafakari/Kuwa katika Jozi/ Kushirikiana

Kutafakari/Kuwa katika Jozi/ Kushirikiana ni mbinu ya haraka ya kumfanya kila mmoja kutafakari na kujadili swali. Hatua hizo ni:

1. Fikiria swali zuri kwa ajili ya majadliano ya wanafunzi. Swali zuri linaweza kuanza kama vile, “je uliwahi… ?” au “je ni afadhali u…?"
2. Wape wanafunzi swali hilo na waambie wafikirie jibu lake.
3. Waambie washirikiane wawili wawili na wajadiliane.
4. Halafu ita jozi mbili au tatu kusoma majibu yao kwa darasa zima.

Ili kuunda jozi za wanafunzi unaweza kuwaambia wanafunzi kuongea na mwenzake aliye pembeni, au anayetazamana naye, au aliye mbele au nyuma yake. Ni vizuri kutofautisha aina ya jozi za wanafunzi. Wanafunzi watafanya vizuri zoezi hili kadiri watakavyokuwa wanajizoeza kufanya.

Njia ya Kutafakari/Kuwa katika Jozi/ Kushirikiana ni vizuri ikafanyika haraka – zoezi zima lichukue kati ya dakika tatu au nne.

Eleza kuwa utakuwa na muda mfupi wa kuchagua mawazo ya kujadiliana kwenye jozi, lakini utaita jozi tofauti kila wakati.

Kuandika/ Kuwa katika Jozi/Kushirikishana

Kuandika/Kuwa katika Jozi/ Kushirikishana ni sawa na Kutafakari/Kuwa katiak Jozi/Kushirikishana lakini wanafunzi kila mmoja wataandika (au kuchora, kama ndo wanaanza kijifunza kuandika) majibu yao kwenye madaftari. Halafu watabadilishana madaftari na wenzake na baada ya kila mmoja kusoma kilichoandikwa watajadili na kuelezea baadhi ya dhana muhimu na kujibu maswali watakayoulizana. Zoezi hili lazima liwe la dakika chache, na mwalimu anaweza kumchagua mwanafunzi mmoja au wawili kusoma darasani kwa sauti kile kilichoandikwa. Kuwahakikishia wengine kuwa watapata zamu ya kusoma kwenye vipindi vingine.

Mwongozo wa Utabiri

Mwongozo wa utabiri ni mbinu ya ufahamu inayotumika mwanzoni mwa kipindi kwa ajili ya kuwafanya wanafunzi watafakari kuhusu mada watakayosikia au kusoma. Mwongozo wa matarajio huwapa wanafunzi hamasa ya kuipenda mada na kuweka malengo ya kusoma na kusikiliza.

1. Kabla ya kipindi kuanza, mwalimu huandaa mwongozo wa matarajio. Hii inamaanisha kuwa anaandika sentensi tano au sita

zinazohusu dhana za msingi kuhusiana na matini itakayosomwa na mwalimu au wanafunzi. Sentensi nyingine ziwe za kweli na nyingine za uwongo. Andaa tungo ambazo majibu yake bado hayajulikani au hayako wazi kabisa. Zichanganye ili zile za ukweli na za uwongo zichanganyike halafu andika kwenye chati kama iliyopo hapo chini, au kwenye ubao. Funika chati hadi hapo utakapokuwa tayari kuitumia. (Kwa wanafunzi wadogo sentensi nne au tano zinatosha; kwa wanafunzi wakubwa zinaweza kuwa zaidi ya hizo).

2. Mfano ufuatao ulitokana na matini kuhusu simba. Sentensi kuonyesha kama tungo ni za kweli au za uwongo ziliwekwa kwenye matini.

Kabla	Kweli? Si kweli? Kabla ya kusoma au kuzungumza, jibu kila swali kwa kuandika K kwa "kweli" au S kwa "si kweli" pembeni ya swali kwenye chumba cha upande wa kushoto.Baada ya kusoma au kusikiliza, jibu tena kila swali kwa kuandikaK kwa kweli au S kwa si kwelibaada ya swali katika chumba upande wa kulia.	*Baada*
	1. Kama ilivyo kwa wanyama wengine jamii ya paka, simba huishi peke yao.	
	2. Simba dume wana manyoya marefu.	
	3. Simba huishi muda mrefu porini.	
	4. Idadi ya simba inapungua.	
	5. Fuvu kongwe kabisa la simba lilipatikana Kenya.	
	6. Simba jike ni wawindaji wazuri kuliko simba dume.	
	7. Ni nadra simba kupumzika.	
	8. Simba huvamia umbali mfupi.	

3. Kabla ya kusoma matini, mwalimu anawaonyesha wanafunzi jinsi ya kutumia mwongozo wa utabiri. Wanafunzi waandike namba 1 hadi 8 (au kutegemeana na tungo zilizopo) kwenye orodha katikati ya kurasa za madaftari yao. Upande wa juu kushoto waandike "kabla", na upande wa juu kulia waandike "baada". Halafu wakati kila tungo inasomwa kwa sauti na mwalimu, kila mwanafunzi anaandike 'Kweli' au 'Si kweli'

kwenye madaftari yao pembeni ya namba ya tungo iliyosomwa, kadiri ya wanavyofikiri wao.

4. Baada ya tungo zote kuandikwa ama *kweli au si kweli* , wanafunzi wafunge madaftari yao na wamsikilize mwalimu akisoma matini kwa sauti. (Wanafunzi wakubwa wanaweza kusoma wenyewe kama kuna nakala za kutosha za matini hiyo). Wakati wa kusomwa matini watakuwa wanasikiliza kwa makini sana kuona kama majibu yao ni sahihi au si sahihi.
5. Baada ya kusoma waambie wanafunzi wafungue madaftari yao na kuandika tena "kweli' na 'si kweli' pembeni ya kila tungo, wakati huu wanaandika upande wa kulia kwenye safu ya 'baada'. Waambie walinganishe majibu yao waliyotoa 'kabla' na 'baada'. Je kuna majibu yoyote yaliyobadilika kutokana na kujifunza baada ya kusikiliza hadithi?
6. Kwa wanafunzi wadogo, au matini ngumu, ni vizuri kupitia tungo hizo kwa pamoja darasani kwa mwalimu kusoma tungo moja kwenye matini na wanafunzi kuweka majibu yao kwenye madaftari yao kabla ya kuhamia tungo nyingine au sehemu nyingine ya matini.

HATUA YA KUKUZA MAARIFA: KUWASAIDIA WANAFUNZI WAJIFUNZE KUTOKANA NA KUSOMA

Baada ya hatua ya matarajio, inakuja awamu ya **kujenga maarifa,** Katika awamu hii, wanafunzi wanaongozwa kuuliza, kujibu maswali yao na kuleta maana. Kuna mbinu mbali mbali za kufundishia ambazo mwalimu anaweza kuchagua ili kutumia katika hatua hii ya somo.

Zoezi la Kusoma kwa Kuongozwa: Vipengele vya Hadithi

Katika zoezi la kusoma kwa kuongozwa: vipengele vya hadithi, mwalimu huigawa matini ya kusomwa kwenye kipindi, katika sehemu nne au tano na kuuliza maswali ambayo wanafunzi watajibu baada ya kusoma kila sehemu. Zifuatazo ni hatua za kufuata.

Hatua ya kwanza: Mwalimu anaichunguza matini na kuona mambo yake ya msingi. Kama ni hadithi, mwalimu atazingatia yafuatayo:

1) sehemu inayoongelea mahali tukio limetendeka, na wahusika wakuu ni akina nani.

2) sehemu inayoongelea tatizo na mahitaji ya mhusika mkuu, au kitendo kinachoanzisha mtiririko wa visa.

3) sehemu inayoongelea jinsi wahusika wanavyofanya ili kujipatia mahitaji yaona kile wanachopambana nacho.

4) sehemu inayofichua suluhisho la kutatua tatizo.

5) sehemu inayoelezea hali ilivyo katika sehemu ya mwisho ya hadithi.

Hatua ya Pili: Mwalimu anapanga maswali ya kuwauliza wanafunzi kabla hajasoma sehemu zote mbili za hadithi. Maswali yawafanye wanafunzi wawe wasikivu na makini ili waweze kujua hoja za muhimu kwa kila sehemu ya hadithi wanachosoma.

Hatua ya Tatu: Mwalimu anawaeleza wanafunzi hatua za kufuatwa. Kabla hawajasoma kila sehemu, lazima wasikilize swali ndipo wasome sehemu inayoofuata kwa ajili ya kupata majibu ya swali walilopewa.

Hatua ya Nne: Watajie swali.

Hatua ya Tano: Wanafunzi wasome sehemu inayofuata.

Hatua ya Sita: Wakumbushe wanafunzi swali na waambie walijibu. Kwa majadiliano zaidi, unaweza kuwaambia wanafunzi wafanye kwanza zoezi la kutafakari/kuwa katika jozi/kushirikiana kabla ya kuwasilisha majibu yao kwa darasa zima.

Zoezi la Kusoma – Kutafakari kwa Kuongozwa: pamoja na Kutabiri

Zoezi la Kusoma – Kutafakari kwa Kuongozwa pamoja na Kutabiri hutumika kwa ajili ya kufanikisha malengo yafuatayo:

a) linawafundisha wanafunzi namna ya kufuatilia matini ya masimulizi, hasa ile yenye visa vya kusisimua;
b) linawapa wanafunzi hamasa ya kusoma kwa umakini;
c) linakuza uwezo wa ufahamu;
d) linaweza kutumika kuwafanya wanafunzi wasome kwa umakini matini watakayoijadili wa kina baadaye.

Katika zoezi la Kusoma – Kutafakari pamoja na Kutabiri, wanafunzi wanasoma hadithi na kutabiri kile kinachoweza kutokea kwenye matini husika. Wanaambiwa wathibitishe ubashiri wao mara kwa mara kwa kurejea taarifa zilizomo kwenye matini, na kutabiri upya. Njia hii ya Kusoma – Kutafakari pamoja na Kutabiri inahitaji wanafunzi wote wawe na matini – ama wawe na kitabu mbele yao au matini iandikwe ubaoni na iwe inasomeka vizuri.

Zoezi la Kusikiliza – Kufikiri pamoja na Kutabiri linaweza kufanyika kwa makundi kuanzia wanafunzi sita mpaka thelathini na zaidi. Wanafunzi wakizidi thelathini watakuwa kikwazo katika ushiriki wa kila mmoja ingawa pia inawezekana kufanyika kwa ufanisi kwa kundi kama hilo.

Matini katika zoezi la Kusikiliza – Kutafakari pamoja na Kutabiri inabidi iwe hadithi nzuri ya yenye visa vinavyoweza kutabirika.: pawepo na tatizo na matiririko wa visa mbalimbali kuelekea kwenye hitimisho.

Muda unaohitajika kwa zoezi hili unategemea na urefu wa hadithi na jinsi mwalimu atakavyotaka wanafunzi wafuatilie hadithi hiyo. Haitakiwi iwe zaidi ya dakika thelathini.

Zoezi la Kusikiliza – Kutafakari pamoja na kutabiri hufuata hatua zifuatazo.
Hatua ya kwanza: Mwalimu huchagua hadithi yenye matukio ya kutabirika ambayo atawasomea darasani.

Hatua ya Pili: Mwalimu huchagua vituo kwenye hadithi ambavyo atasimama – kabla tukio jingine la kwenye hadithi halijatokea or taarifa nyingine muhimu kuhusu wahusika au visa haijajitokeza. Inabidi kuwepo na vituo walau vitano vya kusimamisha mtiririko wa hadithi, la sivyo hamu ya kusikiliza itapungua.

Hatua ya Tatu: Mwalimu anaweza kuanza na kichwa cha hadithi, kuelezea aina ya tanzu ya hadithi (visakale, hadithi za kutunga, ngano, visasili nk), na kuwauliza wanafunzi wabashiri mambo ambayo wanahisi yataweza kutokea kwenye simulizi hilo. Mwalimu anawahimiza wanafunzi kutabiri mambo yanayoweza kuwa ya uhakika zaidi kadiri wanavyoweza na kwa haraka kuyaandika ubaoni. Baada ya kutabiri, mwalimu anawapa changamoto wanafunzi ya kuamua ni jambo lipi ambalo wanaamini lina uwezekano mkubwa wa kutokea kwenye hadithi (hata kama mmoja wao alishabashiri), na halafu wasome kwa umakini ili waweze kuona kitakachotokea.

Hatua ya Nne: Mwalimu anasoma au kusimulia sehemu ya kwanza ya hadithi mpaka alipopanga kusimama, halafu anawauliza wanafunzi waseme ni utabiri upi umekuwa kweli, na ni kwanini wanafikiri hivyo. Halafu wanafunzi wanaombwa kutabiri zaidi, na wanafunzi wanasoma sehemu inayofuata mpaka sehemu nyingine ya kusimama. Hilo zoezi la kutabiri na kuhakikisha walichotabiiri litaendelea mpaka mwisho hadithi itakapoisha.

Hatua ya Tano: Baada ya hadithi kwisha, wanafunzi wanaombwa watafakari kuhusu ubashiri wao. Wanaulizwa ni ubashiri upi umekuwa kweli? Waliwezaje kutabiri hivyo na ikawa kweli? Ni kwa namna ipi uelewa wao kuhusu tanzu husika ya fasihi, mpangilio wa matukio, au maudhui ya hadithi viliweza

kuwasaidia kutabiri kitakachotokea baadaye? Wanatoa ushauri gani kwa wenzao katika kutoa ubashiri ulio sahihi?

KUFIKIRI KWA SAUTI

Njia mojawapo ya kuwafanya wanafunzi wajifunze kusikiliza vizuri na kutafakari vizuri kuhusu kile wanachosikia ni kwa kufuata mfano mzuri wa kuigwa – mwalimu. Unakuwa mfano wa kuigwa pale **unapofikiri kwa sauti**. Kwa kusema kwa sauti kile unachowaza kimya kimya kichwani mwako wakati wa kusoma, unakuwa mfano na kuwasaidia wanafanzi waelewe maswali na mbinu ambazo wasomaji wazuri huzitumia wakati wa kusoma. Kufikiri kwa sauti wakati unasoma maana yake ni:-

- Kufikiria kuhusu swali ambalo mtu anaweza kujiulza kuhusu matini, liseme kwa sauti hilo swali, na wewe mwenyewe useme jinsi utakavyojibu swali hilo.
- Au baada ya kusoma sehemu ya hadithi, sema kile ambacho hadithi inakufanya ufikirie. Halafu sema tukio unalofikiri linafuata
- Au unapokutana na neno ambalo maana yake haiko wazi, unaweza kutumia maneno yaliyotumika pamoja na hilo neno kwa ajili ya kujaribu kutafuta maana yake.
- Au ikiwa wazo limependekezwa au halijaelezwa kwa uwazi, unafikiri kwa sauti kwa lengo la kuunganisha matukio: yaani, kadiri unavyotumia kile unachokijua na kutumia kidokezo kutoka kwenye matini kwa ajili ya kuunda wazo jipya.
- Au wakati mhusika akifanya jambo fulani, unashangaa kwa sauti kwanini alifanya vile. Na unatafuta majibu kujua sababu ya kufanya vile.
- Au wakati unakutana na wazo kuu, sema kwa sauti hilo wazo. Halafu sema kwanini unafikiri wazo hilo ni la muhimu.

- Au unaweza kuuliza aina tatu za viungo vya matini (kwenye kurasa ….): *matini kwa nafsi, matini kwa matini na matini na hali halisi ya ulimwengu*.

Baada ya wanafunzi kuzoea kukusikia ukifikiri kwa sauti, wakaribishe waweze kutoa mawazo yao pia.

KUUNDA TASWIRA AKILINI

Weka vituo vitatu au vinne wakati unasoma kwa sauti hadithi au kipande cha matini na wakaribishe wanafunzi kuunda taswira fulani vichwani mwao kuhusu kile kinachosimuliwa. Wape mapendekezo kwa ajili ya kuwasaidia, na wape pia muda waweze kuhisi hali hiyo. Itasaidia endapo utawaambia wafumbe macho yao wanapounda taswira hiyo.

Ili kuwafanya wanafunzi washiriki zaidi, mwalimu unaweza kupendekeza kuwa wanafunzi wafanye kwa vitendo kwa kutumia miili yao wakiiga vile ambavyo mhusika anafanya kwenye matini, au kuonyesha katika sura zao hisia za mhusika.

Kusoma kwa Kuongozwa

Katika usomaji wa kuongozwa, mwalimu na wanafunzi hupitia matini iliyoandikwa katika kiwango cha usomaji wa wanafunzi.

Lengo. Lengo la usomaji wa kuongozwa ni:-

1) fanya zoezi la kusoma ili kukuza uwezo wa kusoma kwa ufasaha,

2) kukuza ufahamu wa wanafunzi,

3) kujifunza msamiati,

4) kubainisha maneno ya kutumia katikakujifunza msamiati wa lugha.

Utapata wapi matini ya Kusoma kwa Kuongozwa? Matini kwa ajili ya kusoma kwa kuongozwa zinaweza kuwa: -

- Vitabu vilivyotungwa kuendana na viwango vya usomaji wa wanafunzi (kiwango cha usomaji wa wanafunzi maana yake ni kuwa kabla hujafundisha somo hili, msomaji aweze kusoma maneno tisa kati ya kumi bila ya kusaidiwa). Kuwepo na nakala za kutosha za matini ili wanafunzi waweze kuona kwa urahisi;
- Matini unazoandika ubaoni. Matini hizi zinaweza kuwa muhtasari wa vitabu vigumu ambavyo umesoma kwa sauti, au matini za sayansi au maarifa ya jamii au mada yoyote ile;
- “Vitabu Vikubwa” – vitabu vikubwa vilivyoandikwa kwa karatasi ngumu, au vilivyochapishwa mahususi kwa matumizi ya darasani.

Taratibu: Kusoma kwa kuongozwa kunajitokeza katika hatua tatu ambazo ni: hatua ya **maandalizi**, hatua ya **kujenga maarifa**, na hatua ya **kukazia maarifa**.

Katika **hatua ya maandalizi**, mwalimu anachukua dakika kadhaa

- kuwaambia wanafunzi matini inahusu nini.
- waulize wanafunzi wanachojua tayari kuhusu mada husika, na wanachotarajia kukipata;
- kuwaeleza wanafunzi kuhusu msamiati ambao wanaoweza wakawa hawaujui maana yake. Maneno hayo yanaweza kuandikwa ubaoni na kusomwa kwa pamoja. Tumia pia majina ya watu na mahali.

Katika **hatua ya kujenga maarifa**, mwalimu anafanya mambo yafuatayo.

Kukuza ufahamu. Ufahamu maana yake kuelewa kile wanachosoma, kuweza kujenga taswira ya kile wanachosoma, na kuwa na uwezo wa kutafakari kuhusu walichosoma. Mwalimu anakuza uelewa:

- kwa kuigawa matini katika vipande vifupi vifupi, na kuwauliza maswali wanafunzi kabla hawajasoma sehemu nyingine ili

waweze kutambua dhumuni la kusoma. Mwalimu anaweza kusema kuwa: “Hadithi hii inamhusu kijana mmoja anayeitwa Toe. Soma sehemu ya kwanza ili tujue mahali ambapo Toe anaishi na akina nani anaishi nao.”

- Kwa kuwauliza wanauliza wanafunzi watoe maoni yao kuhusu kile walichokisoma. Kwa mfano, “Ungejisikiaje kama ungekuwa Toe?” “Je ungeweza kufanya hivyo na wewe?”
- kwa kuwauliza wabashiri kitakachotokea kwenye hadithi (kama hawaijui hiyo hadithi kabla). “Unafikiri nini kitatokea?” “Kwanini unafikiri hivyo?”
- Kwa kuwauliza wanafunzi wajenge taswira kwenye akili zao kuhusu kile wanachosoma. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuuliza, “Elezea jinsi tukio lilivyokuwa kwenye kizuizi”. Tukio hilo likoje? Nani wako hapo? Wamevaaje? Watu wanajisikiaje wanapofika hapo? Wanakuwa na tabia gani ?

- **Kujenga uweza wa kusoma kwa ufasaha.** Kusoma kwa ufasaha maana yake ni kutamka maneno kwa urahisi na kwa haraka pasipo kukwama. Inamaanisha watu wanasoma kwa mwendo wa kawaida – siyo kwa taratibu sana. Inamaanisha kuwa wanasoma kwa kuigiza – wanaonesha kuwa wanielewa matini. Mwalimu anakuza usomaji fasaha—
  - kwa kuwaalika wanafunzi kusoma sentensi tena na tena, “kufanya ionekane kama unaongea na sisi”.
  - Kwa kuwakumbusha wanafunzi kusoma na kuigiza. Kwa mfano, mwalimu anaweza kusema, “Tafadhali soma tena. Na mfanye mvulana aonekane kama anatania”; au soma tena sehemu ile na ifanye kama kweli inatisha”.

- **Kufundisha msamiati.** “Msamiati” inamaanisha maana ya maneno. Lakini maneno yanaweza kumaanisha vitu tofauti kutegemeana na muktadha tofauti: kwa mfano, “paa” kama jina la mnyama na kama kitendo cha

kwenda juu angani. Tunaweza kufundisha msamiati kwa kuwakumbusha wanafunzi maneno tuliyoyadokeza awali. Au tunaweza kufafanua maana ya maneno mapya wakati wanafunzi wanakutana nayo wakati wa kujisomea. Au tunaweza kuwaambia wanafunzi kuelezea sentensi walizosoma kwa maneno mengine kwa ajili ya kuweka maana iwe wazi zaidi.

Katika hatua ya kukazia maarifa, mwalimu anaweza kufanya mambo kadhaa:

- Waalike wanafunzi kusimulia tena hadithi au matini waliyosoma;
- waombe wanafunzi kujibu maswali ya mjadala yanayoanza na “kwanini…”, “endapo…”, “lipi lilikuwa jambo muhimu kuhusu…” na “je hadithi imekufanya ufikirie kuhusu jambo gani?”
- waulize wanafunzi waigize kuhusu visa vilivyosimuliwa kwenye hadithi, huku wanafunzi wengine wakitoa maoni ya kusaidia kuboresha.
- Waombe wanafunzi waandike majibu yao kutokana na walichokisoma.

Kuvuna Maneno. Ili uweze kukusanya maneno kwa ajili ya kuweka kwenye ukuta wa maneno na baadaye kujifunza msamiati, mwalimu anaweza kuvuna maneno kutokana na zoezi la kusoma kwa kuongozwa, akitilia mkazo kwenye neno kusoma kwa sauti kama linavyoonekana. Ndipo mwalimu anaweza kuandika neno hilo kwenye karatasi au karatasi ngumu na kubandika kwenye ukuta wa maneno. Maneno manne au matano kutoka katika kila zoezi la kusoma yanaweza kuvunwa kwa njia hii.

Maneno yapi? Ni wazo zuri kupitia mpangilio wa maneno kwa ajili ya kujifunza msamiati kwenye sehemu inayofuata ya Kujifunza Msamiati ili kuweza kuamua ni maneno yapi muhimu kwa wanafunzi kujipimia.

HATUA YA KUKAZIA MAARIFA: KUTUMIA MAANA INAYOTOKANA NA MATINI

Wanafunzi wanaofikiri kwa kina hufanya zaidi ya kuelewa matini. Wakishaielewa, wanaweza kuchukua maana na kuijadili, kuitafsiri, kuitumia au kufanya mdahalo. Kuna mbinu kadhaa ambazo mwalimu anaweza kuchagua ili kutumia wakati wa kukaza maarifs

Kurudia Kusimulia Matini

Kurudia kusimulia hadithi si tu kwamba inawasaidia wanafunzi kuimarisha uwezo wao lakini pia inawasaidia kujifunza kuhusu muundo au mifumo ya katika hadithi.

Baada ya wao kusoma hadithi nzima, unaweza kuwauliza wasimulie tena kuhusu kilichotokea. Waambie wasimulie hatua kwa hatua kadiri ya jinsi matukio yalivyotokea. Unaweza kuwauliza maswali yafuatayo kwa ajili ya kuwasaidia katika kukumbuka:

"Nani ataniambia---

1. *Hadithi inamhusu nani?*
2. *Hadithi hii imetokea wapi?*
3. *Mhusika mkuu alitaka nini au alitaka kufanya nini?*
4. *Kitu gani cha kwanza kutokea?*
5. *Baada ya hapo kilifuata nini?*
6. *Na nini kilitokea baada ya hapo?*
7. *Na mwishowe kulitokea nini?*
8. *Na hatimaye mwisho wa hadithi kumetokea nini kwa mhusika mkuu?"*

Njia nyingine, unaweza kuandika ubaoni matukio ya hadithi pasipo kufuata mtiririko wake huku kila sentensi moja ikiwakilisha tukio moja. Weka namba kwa kila sentensi. Waambie wapangilie vizuri sentensi hizo kwa kufuata mtiririko wa matukio. Mfano ufuatao umetokana na hadithi ya *Tabu wa Taire.* Kwa ajili ya kusaidia usimuliaji, unaweza kuandika ubaoni yafuatayo:-

1. Mpiga ngoma anaonekana kufika katika kijiji cha Tabu.
2. Mpiga ngoma alipita kila mji huku akipiga ngoma.
3. Siku moja Tabu alikimbia na kujificha msituni.
4. Tabu aliimba akiwa ndani ya ngoma.
5. Ndugu zake Tabu walimsikia akiimba na wakamtoa ndani ya ngoma.
6. Tabu hakuweza kufanya kazi yoyote nyumbani.
7. Mpiga ngoma alipita karibu na kumtia ndani ya ngoma yake kubwa

(Mpangilio sahihi ni 6, 3, 7, 2, 1, 4, 5).

Halafu soma kila sentensi na waulize wanafunzi wataje mpangilio wanaoona ni sahihi.

Baada ya sentensi kupangiliwa vizuri, waombe wanaotaka kujitolea kusimulia tena hadithi.

Mpangilio wa Hadithi

Ukitaka kusisitiza vipande vya matukio kwenye hadithi, unaweza kuandika ubaoni mpangilio wa hadithi, kama hivi hapa.

Mtu fulani…	

Alitaka …	
Lakini…	
Kwahiyo…	
Na baadaye…	

Baada ya wanafunzi wamesharudia kusimulia hadithi, waambie wakusaidie kufikiria sentensi za kuweka katika kila sehemu. Baada ya wanafunzi kufanya zoezi la kurudia kusimulia hadithi kwa mapangilio huo wa usimuliaji, wanaweza kuruka kipengele cha kurudia kusimulia na wakaenda moja kwa moja kwenye mpangilio wa hadithi.

Kutafuta Wazo Kuu

Kutafuta wazo kuu ni kipengele muhimu katika kuelewa matini. Ili kuwasaidia wanafunzi kutafuta wazo kuu kwenye matini unaweza kuwapatia sentensi mbili au tatu halafu waulize wachague ile iliyo nzuri zaidi na waulize waeleze kwanini wanaona ndio nzuri zaidi. Zifuatazo ni hatua za kufuata kwa zoezi hili.

Kabla ya kipindi, soma hadithi kwa umakini na chagua wazo kuu. Andika sentensi moja au sentensi kadhaa zinazoelezea kwa kifupi hadithi inahusu nini. Kwa mfano, kwa hadithi ya *Tabu wa Taire*, wazo kuu linaweza kuwa, “msichana anajifunza kuwa unakuwa mwenye furaha kama unakuwa mtoto mzuri ndani ya familia”.

Halafu andika sentensi nyingine mbili ambazo haziongelei wazo kuu. Ziongelee suala jingine ambalo limegusiwa kwenye hadithi lakini si wazo kuu. Kwa mfano, “mpiga ngoma alikuwa mnene na mwenye sura mbaya”, na “Tabu hakuwa na furaha ndani ya ngoma”.

Baada ya kusoma hadithi darasani soma sentensi tatu ulizoandaa: moja inaongelea wazo kuu na nyingine zinaongelea mambo yasiyo na umuhimu sana. Ziandike sentensi hizo ubaoni. Halafu zisome pasipo mpangilio kama hivi:

1. Mpiga ngoma alikuwa mnene na mwenye sura mbaya.
2. Tabu hakuwa na furaha ndani ya ngoma.
3. Msichana alijifunza kuwa unaweza kuwa mwenye furaha kama unakuwa mtoto mzuri ndani ya familia.

Watake wanafunzi waeleze sentensi wanayofikiri ni wazo kuu la hadithi.

“Mchezo wa Kuchora ”

“Mchezo wa kuchora” ni njia ya wanafunzi kusema wanachofikiri ni cha muhimu ndani ya hadithi kwa njia ya kuchora. Pia mchezo huu unawapa nafasi wanafunzi ya kuongelea mawazo muhimu au dhamira zilizomo kwenye hadithi.

Hatua za “Mchezo wa Kuchora” ni hizi:

1) Wasomee kwa sauti wanafunzi hadithi au matini yeyote.
2) Waambie wanafunzi wachore picha inayoonyesha walichofikiri ni cha kufurahisha na cha muhimu kutokana na walivyosikia. Wanaweza kuchora picha kwenye madaftari yao.
3) Waweke wanafunzi katika makundi ya wane au watano – ama kwenye dawati moja, au kwa kuzunguka darasani na kuunda makundi ya wanafunzi.

4) Wanafunzi wanafungua madaftari yao na kuyaweka juu ya dawati, na mmojawapo anayakusanya yote na kuyachanganya na hivyo hakuna anayeweza kulitambua daftari lake.
5) Kila mwanafunzi anachukua picha ambayo si ya kwake.
6) Wanafunzi wanaziangalia kwa makini picha hizo.
7) Kila mmoja kwa wakati mmoja anatoa tafsiri ya picha aliyochagua – yaani wanawaambia wenzao kile kinachoelezwa kwenye picha na jinsi inavyosimulia matukio muhimu ya kwenye hadithi au mawazo muhimu ya hadithi.
8) Aliyechora picha hiyo inabidi akae kimya wakati huo wa kuwasilisha darasani.
9) Baada ya mawasilisho, mchoraji anaongelea kwa kifupi sana vitu vichache kuhusu picha yake.
10) Kama muda utakuruhusu, mwalike mwanafunzi mmoja au wawili wasimame na kutoa tafsiri ya hiyo picha mbele ya darasa zima (Ni sawa tu ikiwa kuna baadhi hawataweza kuiona hiyo picha – wanaweza kuendelea kusikiliza tafsiri yake)

Ukweli mara mbili na Uongo mara moja

Hii ni njia ya haraka na iliyozoeleka sana ya kukazia maarifa kwa ajili ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wamesoma kwa umakini na kuelewa hadithi na matini wanazokutana nazo darasani.

1. Wakati wa maandalizi, mwalimu anatunga sentensi tatu au tungo ambazo zinaendana moja kwa moja na yale yaliyomo kwenye hadithi au habari ambayo wanafunzi watasoma. Sentensi mbili ya hizo ziwe

za kweli na moja ya uongo. Hizo zote ziwe zimeandikwa kwa maandishi makubwa kwenye chati au ubaoni na kufunikwa mpaka muda wa kutumika ukifika.

2. Baada ya hadithi au matini kusomwa waambie wanafunzi waandike namba 1, 2, na 3 kwenye madaftari yao. Sasa waonye kuwa wasiwape majibu yao wenzao humo darasani, na waambie kuwa utawapa sentensi tatu, mbili zikiwa za kweli na moja ya uongo. Soma kila sentensi kwa sauti. Waelekeze wanafunzi “ukweli’ kwenye madaftari yao pembeni ya namba mbili wanazoona za kweli na “uongo” kwenye namba ambayo si ya kweli.

3. Waalike wanafunzi kubadilishana na kulinganisha majibu yao na mwenzake aliyekaa naye karibu, na toa sababu kwanini uongo inasemekana kuwa ni uongo.

4. Kwa wanafunzi wadogo au wanaoanza kujifunza kusoma sentensi zinaweza kuwa za moja kwa moja, zikifanana moja kwa moja na kile kilichoandikwa kwenye matini. Kwa wanafunzi wakubwa au wazoefu wa kusoma, sentensi zaweza kuwa ngumu kiasi, zikiwataka kufanya marejeo na kuunganisha na taarifa inayoashiria na siyo ambayo imeelezwa au kutajwa moja kwa moja.

Kuigiza

Kuigiza ni njia ya asili ya kuwafanya wanafunzi kuchunguza maana ya hadithi waliyosikia ikisomwa kwa sauti au waliyosoma wenyewe. Kwa njia ya zoezi hili, wanafunzi watatunga hadithi – yaani watakuwa wakiandaa sentensi zao wenyewe kwa ajili ya kusimulia. Hata kama hawatazikariri hizo sentensi mapema, ni vizuri kufanya mazoezi ya kile watakachosema baadaye.

Zifuatazo ni hatua za kufuata wakati wa kuigiza.

1. **Kufanya mazoezi ya hadithi.** Ni vizuri sana kama wanafunzi watafanya mazoezi ya kurudia kusimulia hadithi kama hawajaigiza ili kila mmoja aweze kuwakumbuka vizuri wahusika na mtiririko wa visa vya hadithi.

2. **Kuteua wasimuliaji**: Wasimuliaji ni wale watakaosimulia sehemu za hadithi ambazo hazitaigizwa. Kama wanafunzi ni wakubwa basi unaweza kuchagua mwanafunzi mmoja au jozi ya wanafunzi watakaokuwa wasimuliaji (msimuliaji namba 1 na namba 2). Lakini kama wanafunzi bado hawako tayari kufanya hivyo, utatakiwa kufanya mwenyewe. Ukishafanya mwenyewe kama msimuliaji wa hadithi kadhaa, itawezekana sasa baadhi yao wakajitokeza mbele ya darasa na kuwa wasimuliaji.

3. **Kupanga wahusika:** Kunahitajika kuwa na wahusika kwa nafasi muhimu kwenye hadithi, na wahusika wajenzi kama vile umati wa watu, wanakijiji na kadhalika. Yawezekana si kila mwanafunzi akawa na jukumu la kufanya kwahiyo chagua wanafunzi kuwa na majukumu tofauti. Kwa njia hiyo kila mmoja atapata nafasi ya kuigiza muda fulani.

4. **Kuamua sehemu za kuigizwa na za kusimuliwa.** Kama hadithi, kwa mfano, ni ya *Tabu wa Taire*, unaweza kuigiza:-
    a. Mama yake Tabu’ akiwaagiza mabinti zake kufagia uwanja. Mabinti wengine wanakubali lakini Tabu anagoma.
    b. Tabu yuko ndani ya ngoma huku mpiga ngoma akitembea kijijini, mpiga ngoma anacheza ngoma huku Tabu akiimba taratibu
    c. Mpiga ngoma anacheza katika kijiji cha akina Tabu, na Tabu anaimba kwa shida, na dada zake wanaitambua sauti yake.
    d. Tabu anaokolewa na kutolewa kwenye ngoma na babake.

Unaweza kuamua kuwa wanafunzi wakaigiza sehemu chache kuliko hizi au zaidi ya hizi kutegemeana na muda ulio nao. Sehemu zile ambazo hazitaigizwa zitasimuliwa na msimuliaji au wasimuliaji.

5. **Waigizaji kufanya mazoezi ya kila tukio huku ukielekeza.** Unaweza kuwaelekeza kwa kuuliza maswali. “Dada zake Tabu wanajisikiaje wanaposikia sauti ya Tabu? Wanafanyaje?”

6. **Kuigiza kwaajili ya wengine?** Wanafunzi hufurahia sana kuigiza ikiwa tu wataigiza hadithi mbele ya wengine. Lakini kwa upande mwingine, kama lengo lako ni kutumia igizo kutafuta maana ya hadithi, unaweza kuamua usijichoshe sana na kuigiza na kusisitiza zaidi kutafakari wakati wa kuigiza. Uamuzi ni wako.

Angalizo kwa Mwalimu: Njia moja ya kuanza ni kwa kuonyesha kupitia kundi moja likiwa mbele ya darasa, na wengine wakiwa watazamaji. Wanafunzi wakishazoea hatua za kuigiza, washirikishe wote kwa kugawanywa kwenye makundi, huku kila kundi likiwa na wanafunzi wengi wa kutosha kulingana na wahusika na wasimuliaji katika hadithi. Makundi hayo baadaye yanaweza kuwekwa katika jozi ili kila moja liigize mbele ya mwenzake. Ingawa njia hii inahitaji matumizi mazuri ya nafasi darasani kama wako wengi, inatoa nafasi wa wanafunzi wote kushiriki kikamilifu kama washiriki na si watazamaji.

Kila mmoja Anaongoza: Kuigiza kwenye Madarasa Makubwa

Mbinu hii inasaidia kusimamia uigizaji na kuwafanya wanafunzi wote wafikirie kwa kina kuhusu wahusika na matukio kwenye hadithi.

Uzuri ni kwamba inafanya kazi vizuri kwenye madarasa makubwa au yenye wanafunzi wengi.

1. Baada ya hadithi kusomwa kwa sauti, au wanafunzi kumaliza kuisoma wenyewe, waambie wabainishe vipengele muhimu kwenye hadithi vinavyofaa kuigiza. Baada ya majadiliano, kipengele kimojawapo huchaguliwa kwa kuigizwa.
2. Kinachofuata ni kumtafuta aliye tayari kujitolea au chagua mwanafunzi kwa ajili ya kila mhusika kwenye igizo husika.
3. Waambie hao wanafunzi wasogee mbelee ya darasa na wachukue nafasi zao yake ya kuigiza.
4. Huku ukionyesha kwa kila mhusika kwa zamu, waulize wanafunzi wengine darasani wapendekeze wanadhani mhusika huyu anafikiri au anahisi nini kwa wakati huo katika hadithi: *lengo lao ni lipi? Kipi kinawaogopesha? Wanawafikiriaje wahusika wengine kwenye tukio? nk.* Lengo ni kuwasaidia wanafunzi kutafsiri vizuri matukio kwa mtazamo wa mhusika huyo na kutafakari kwa kina kuhusu mahusiano na matatizo ambayo yanaweza yasiwe wazi sana kwenye matini husika. Hili likiwa linatokea, mwanafunzi anayechukua nafasi ya mhusika anayejadiliwa awe anasikiliza pasipokusema chochote. Lengo ni kuwapa waigizaji mawazo ambayo wataweza kuchagua ili kuamua waigizeje kwa nafasi wanayowakilisha.
5. Kwa mara ya kwanza unaweza kuhitaji kutengeneza maswali yatakayowafanya wanafunzi waweze kutafakari kuhusu mwelekeo ambao hawakuufikiria wao wenyewe. Hamasisha wanafunzi darasa zima watoe mapendekezo.
6. Baada ya kuzingatia msimamo na mtazamo wa kila mhusika wape waigizaji walioko jukwaani dakika moja au mbili za kujadiliana kuhusu tukio, na ndipo uwaambie waanze kuigiza

darasani. Huku wakitakiwa kuwakilisha matukio halisi ya kwenye hadithi, waigizaji watakuwa huru kutumia maneno yao wenyewe kueleza mawazo yao kadiri inavyowezekana.

7. Kufuatia uigizaji huo, waambie wanafunzi wajadili na watoe maoni yao kuhusiana na mazingira ya uigizaji kwa kutumia njia ya Kutafakari/Kuwa katika Jozi/Kushirikishana.

Kuuliza “Maswali ya Kutafakari”

Katika sehemu iliyotangulia tulipojadili kuhusu “Kufikiri kwa sauti” tulipendekeza njia nyingi ambazo mwalimu anaweza kuzutumia kutafakari kuhusu matini. Wazo lilikuwa kuwaonyesha wanafunzi jinsi watu makini wanavyofikiri kuhusu wanachosoma. Baada ya kuisoma matini kwa sauti unaweza kuwauliza wanafunzi maswali ambayo yatawapa changamoto ya kutafakari zaidi kuhusu walichosikia punde.

Njia mmojawapo ya kufikiri kuhusu maswali mazuri ya kutumia ni njia ya mkato kuhusianisha:
Matini kwa mtu binafsi
Matini kwa matini
Matini kwa mazingira halisi ya dunia

Yaani--

- Ni nini _____ (kilichoandikwa kwenye matini) kiliwafanya wafikirie kuhusu maisha yao? (*Matini kwa mtu binafsi).*
- Ni nini _____ (kilichoandikwa kwenye matini) kiliwakumbusha kuhusu kitu walichowahi kusoma mahali pengine (*Matini kwa matini*), na

- Ni nini _____ (kilichoandikwa kwenye matini) kiliwakumbusha kuhusu matukio halisi katika maisha *(Matini na mazingira halisi ya dunia).*

Tofauti za Kitaaluma (Mjadala wa Kina)

Njia hii inawasaidia wanafunzi kuwa na msimamo na kuutetea kwa kujenga hoja zenye mashiko. Inawasaidia kujizoeza kutoa hoja kwa ustaarabu, kutafakari kuhusu hoja husika au hoja kutoka upande zaidi ya mmoja na kujenga hoja zenye ushawishi. Ni njia bora sana ya kuwasaidia wanafunzi wakubwa kujieleza, kusikia maoni ya wenzao darasani, na kukuza uwezo wa kufanya maamuzi sahihi kuhusiana na masuala yanayoibuliwa kwenye hadithi au matini wanazosoma darasani.

1. Anza kwa kuwaweka wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wapendekezee swali au suala linaloibua mjadala na walijadili. **Ni muhimu swali likawa na majibu ya "ndiyo" au "hapana" – au tungo inayojibiwa kwa "kukubali" au "kukataa" – na kuwa ama jibu liweze kuwa lenye hoja au lisiwe na hoja.** Swali liendane na mada na matini ambazo wanafunzi wanazisoma sasa.

2. Wape wanafunzi dakika chache za kuanza majadiliano kuhusu swali au sentensi kwenye makundi ya wanne ili kuhakikisha wote wanaelewa kinachomaanishwa na kwanini ni muhimu.

3. Halafu waambie wanafunzi wajihesabu kwenye makundi yao kuanzia 1, 2, 3, na 4. (Kama kundi moja lina wanafunzi watano, basi yule wa tano atachukua namba 1 kwahiyo wawili watakuwa na namba 1).

4. Waambie kuwa wale waliopewa namba 1 na 2 watakuwa wanajibu “Ndiyo” (au “kukubali”); na wale wenye namba 3 na 4 watakuwa wakijibu “Hapana” au “Kutokubali”.

5. Sasa ielekeze kila jozi ndani ya kila kundi waendelee wenyewe, wachukue karatasi na kalamu, watumie dakika tano kuorodhesha sababu za kusimamia mawazo yao, bila kujali yakoje.

6. Sasa ni hatua ya nzuri zaidi: baada ya dakika nne au tano unataja muda. Sasa mwambie kila mtu ajiandae kutoa hoja, wale wa upande wa “Hapana”, (Namba 3 na 4) waambie wakae chini popote pale walipo. Halafu waambie wale wanaosimama (Namba 1 na 2) watazamane na mwingine aliyesimama, lakini awe si Yule mwenzake kwenye jozi. Waonyeshane vidole ili kuhakikisha kuwa ndio watakaokuwa pamoja kama jozi – lakini wasiondoke. Waambie wakae pale walipo, na wale wengine waliokuwa wamekaa (namba 3 na 4) wasimame. Na wao pia waonyeshe wenzi wao kwa kuwanyooshea vidole. Waambie watakuwa na dakika nne za kusikiliza sababu za mwenzake na kuziandika zile ambazo hawakuwa nazo mwanzoni. **Halafu waambie kuwa sasa waungane na wenzao wapya na wabadilishane sababu zao.**

7. Baada ya dakika nne au tano wajulishe muda tena.

8. Waambie warudi kwa wenzao wa mwanzo kabisa na kubadilishana sababu walizopata kwa wenzao wapya huku wakiunganisha na sababu ambazo tayari walikuwa nazo.

9. Halafu waambie kuwa wafikiri kwa makini kuhusu sababu zilizotolewa zinazotetea msimamo wao. Wajiandae kwa mdahalo na jozi nyingine ndani ya kundi moja la wanne. Sasa, ili wajadliane, wanatakiwa

wawe na sentensi zinazosimamia msimamo wao na sababu nzuri mbili au tatu za kutetea huo msimamo wao. Wape wanakundi dakika nne au tano kufanya hivyo.

10. Wakiwa tayari kwa majadiliano, waambia jozi moja iungane na nyingine kwenye kundi na waanze majadiliano. Ili waweze kujadiliana, upande mmoja unatoa kauli yake na sababu za kutetea kauli hiyo, na upande mwingine hivyohivyo. Ndipo wanajadili hoja za kila upande na kufikia hitimisho.

11. Sasa linakuja suala la kubadili upepo wa mjadala. Uache mjadala uendelee kwa dakika sita au saba. Kisha waambie kuwa wako huru kuachana na msimamo wa makundi yao na watoe hoja zao binafsi wanazoamini ni za kweli.

12. Waambie kuwa kwa makundi yao wajaribu kufikia mwafaka: yaani, wote wakubaliane na upande ambao watapenda kuwepo na sababu za kutetea upande huo.

13. Baada ya dakika nne au tano, mwite mtu mmoja kwa kila kundi ili aeleze msimamo wa kundi uliotokana na majadiliano waliyofanya.

Mstari wa Msimamo/Thamani

Mbinu hii inawasaidia wanafunzi kubaini “ni upi msimamo wao” kuhusu masuala ambayo yana aina tofauti za majibu. Inawasaidia pia kuwajengea uwezo wa kutoa hoja zenye mashiko kwa ajili ya kusimamia nafasi yao.

Zifuatazo ni hatua za kufuata:

1. Toa darasani kauli inayofikirisha ambayo ina majibu mbalimbali, kuanzia na “kukubaliana kabisa” hadi “kutokubaliana kabisa” na hoja nyingne zote za katikati.

2. Wape wanafunzi dakika tatu au zaidi ili waweze kuiangalia kauli hiyo na kuandika majibu yao (Kukubali kabisa, kukubali kiasi, kukubali na kutokubali, kutokubali, kutokubali kabisa nk.).

3. Sasa simama upande moja wa darasa na tangaza kuwa unawakilisha nguzo moja au upande wa mwisho kabisa wa msimamo kuhusiana na kauli husika. Elezea msimamo wako kwa ujasiri na kwa ufasaha na toa sababu moja au mbili kwanini unaamini msimamo wako ni sahihi.

4. Mwite yeyote ajitolee kusimama upande mwingine wa darasa na awe msimamo tofauti. Wahimize kutoa sababu nzito, zenye ushawishi mzito wa kutetea kauli zao.

5. Sasa waambie wanafunzi wafikirie mstari kati yenu wawili (pande mbili zenye misimamo mikali inayopingana kuhusu mada hiyo) na waende wasimame kwenye mstari huo upande ule wanaohisi maoni yake yanaendana na ya kwao.

6. Wanafunzi wanatakiwa kulinganisha maoni yao na ya wale wa upande mwingine ili kuhakikisha kuwa wamesimama katika upande sahihi. Baada ya kuwasikiliza wengine na kueleza ya kwao, baadhi yao wanaweza kuamua kubadilisha upande au kubaki na upande wao.

7. Baada ya wote kupata muda kujadili hoja zao, waambie wanafunzi wakiwa katika mistari yao wawaambie wenzao humo darasani kuhusu wanachofikiri na sababu zao za msingi kutetea msimamo wao.

8. Unaweza kufuatilia zoezi kama fursa nzuri ya kuandika kwa wasikilizaji kuandika wanachofikiria kuhusu suala hilo na sababu zao. Kwa njia hii

mstari wa msimamo utasaidia kufanya mazoezi ya kuandika insha ya hoja zenye mashiko au yenye lengo la kushawishi.

Kuelewa Matini za Habari

Kuelewa matini za habari kunahitaji mbinu za ufahamu tofauti na zile za kuelewa matini za masimulizi. Njia tatu za : **kujua/kutaka kujua/kujifunza, usomaji wa jozi/ufupishaji wa jozi,** na **Kufundishana** zipo kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi kuelewa matini za kuhabarisha.

Kujua/kutaka kujua/kujifunza

Zoezi hili linaweza kutumika kuunda somo zima. Linawataka wanafunzi wafikirie nini wanajua kuhusu mada ya somo, waulize swali kuhusu mada hiyo na watafute majibu ya maswali hayo. Ujifunzaji wa vitendo ni bora kuliko ule usio wa vitendo. Wanafunzi hujifunza vizuri zaidi iwapo :

1) wanakumbuka kile wanachojua
2) wanauliza maswali
3) wanathibitisha uelewa wao

Njia hii inawaelekea wayafanye mabo hayo matatu.

Hatua ya 1 : Anza kwa kutaja mada na kuwataka wanafunzi wafikirie kuhusu nini wanajua kuhusu mada hiyo. Ni vizuri wanafunzi waorodheshe mawazo yao na kushirikishana kabla ya kujibu

Hatua ya 2 :Unda jedwali katika ubao au karatasi ngumu

Hatua ya 3 : Waambie wanafunzi waseme nini wanajuaa kuhusu mada. Andika mawazo yao kwenye safu ya **Nini tunajua ?** Unaweza kupangilia mawazo yao kwenye makundi kwa jinsi unavyoyapokea.

Hatua ya 4 : Sasa waambie wanafunzi wafikirie maswali waliyonayo kuhusu mada. Wanaweza kuanza kwa kupitia wanachojua, na kutafuta maeneo ambapo ufahamu wao haujakamilika. Andika maswali yao kwenye jedwali kwenye safu ya **Nini tunataka kujua ?** Uwe huru kuongeza maswali yako

Hatua ya 5 : Wanafunzi sasa wasome matini(au wasikilize mhadhara, au wafanye uchunguzi wa aina fulani). Wanakumbushwa kutafuta majibu ya maswali yao na mawazo yoyote mapya ambayo hawakuyafikiria.

Hatua ya 6 : Wanafunzi wawasilishe mambo waliyojifunza kutoka kwenye matini. Kwanza wawasilishe majibu waliyopata kwa maswali yao, ksha wanawasilisha mawazo yoyote muhimu na ya kuvutia waliyogundua. Mwalimu aweke rekodi ya mawazo hayo kwenye jedwali katika safu ya **Ni nini tumejifunza ?**

Usomaji katika jozi/ufupishaji katika jozi

Mbinu hii huwawezesha wanafunzi katika jozi kusoma matini kwa makini ili waielewe. Kam ilivyo katika mazoezi mengine ya ujifunzji wa kushirikiana, mbinu hii inawawezesha wanafunzi kufanya juhudi zaidi katika ujifunzji wao na wa wengine. Njia hii imekusudiwa kuhamasisha namna tofauti ya kufikiri ambazo zote zinahamasisha ufahamu.

Usomaji katika jozi/ufupishaji katika jozi huchukua urefu wa mara tatu mpaka nne ya kusoma matini kwa sauti. Ili kuokoa muda, unaweza kuwataka wanafunzi wafanye usomaji katika jozi kwa aya nne mapka sita za mwanzo, na kisha kila mmoja some mwenyewe sehemu iliyobakia.

Hatua ya 1 : Chagua matini inayohabarisha na ya urefu wa kutosha. Iwe na aya fupi (si zaidi ya sentensi tatu kila moja), au uikate katika sehemu ndogo.

Hatua ya 2 : Kama wanfunzi ni wageni katika utaratibu huu, uonyeshe mfano kwanza

a. Soma habari kwa sauti na utoe ufupisho wake. Elezea kuwa hii ni kazi moja katika zoezi hili. Elezea sehemu za ufupisho : ni mfupi kuliko habari yenyewe, lakini una mambo yote ya muhimu.
b. Waulize wanafunzi maswali mawili kuhus matini . Elezea kuwa hili ni jukumu lingine katika zoezi hili

Hatua ya 3 : Waambie wanafunzi wakae katika jozi. Eleza kuwa mwanafunzi mmoja atasoma aya ya kwanza au sehemu iliyowekwa alama katika matini na kisha atatoa ufupisho wake, kama ulivyoonyesha kwenye mfano. Wape muda ili kila mmoja afanye. Kisha pima uelewa kwa kuwataka wanafunzi kadhaa kutoa ufupisho wao. Toa mapendekezo inapobidi. Sasa waambie wanafunzi wengine kuuliza mswali kuhusu kifungu cha habari. Baada ya kupata nafasi ya kufanya hivyo, pima uelewa kwa kuwaambia wanafunzi kadhaa kutoa maswali yao. Toa mapendelkezo tena kwa ajili ya kuboresha pale inapobidi.

Hatua ya 4 : Wanafunzi wakishaelewa utaratibu, waendelee kusoma wenyewe, kufupisha na kuuliza maswali kuhusu matini katika kila kifungu cha habari. Wakumbushe kubadilishana majukumu baada ya kusoma na kujadili kila kifungu.

Tafakari : Usomaji katika jozi na ufupishaji katika jozi ni njia nzuri kuwafanya wanafunzi wasome kwa makini matini ngumu.

Kufundishana

Katika kufundishana, mwalimu anaonyesha mfano wa namna ya kuelewa matini habarishi kwa kutumia mfululizo wa hatua za ufahamu : ufupisho, kuuliza maswali, ufafanuzi, na utabiri. Baada ya mwalimu kuonyesha mfano wa mchakato huu katika

hatua nne, wanafunzi kwa zamu wafuate hatua hizo hizo na kuwaelekeza wengine kujadili vifingu vya habari vilivyosomwa.

Zifuatazo ni haut akatika ufundishanaji :

1. Mwalimu anagawanya habari ya kusomwa katikasehemu fupi fupi kutegemea na urefu wa habari yenyewe, aya tatu au nnezinaweza kutosha.
2. Mwalimu anamwambia kila mmoja asome habari kimya
3. Baada ya kumaliza kusoma, mwalimu aonyeshe mchakato wa ufahamu kwa kufuata hatua nne zifuatazo :

    a. **Fupisha** sehemu katika sentensi moja au chache
    b. Waulize kikundi **swali moja au mawili,** epuka maelezo ya kina sana
    c. Bainisha sehemu ya habari iliyo ngumu na **fafanua** kwa kuelezea, kutoa mifano, kuchora mifanano, au kutoa maelezo mengine yanayofafanua
    d. **Tabiri** sehemu inayofuata itakuwa kuhusu nini au nini cha kujifunza katika sehemu hiyo.

Mwalimu arudie hatua ya 1 mpaka ya 3 mpaka imeeleweka na wanafunzi wote. Kisha anweza kufanya zamu ya kuongoza mjadala kwa hatua zilizotajwa : mwalimu-mwanafunzi-mwalimu-mwanafunzi au mwalimua-mwanafunzi-mwanafunzi. Mwalimu kuendelea kuonyesha mfano na kushiriki ni muhimu kwa mafanikio ya wanafunzi katika utaratibu huu.

.

Mbinu ya Sita : Msamiati

Kama tunavyojua, maneno ndiyo msingi wa ufahamu. Msomaji na msikilizaji mzuri huwa na msamiati kichwani mwake ambao unafanana sana na msamiati anaokutana nao wakati wa kusoma na kusikiliza. Pia anakuwa na mbinu za kutambua muktadha wa matumizi ya maneno unaomwezesha kupata dhana nzima za maneno ambayo alikuwa haijui kabla.

Zifuatazo ni mbinu za kuwasaidia wanafunzi wajifunze msamiati

1) **Kutafuta maneno yaliyokwisha kutajwa awali.** Unaweza kuwakumbusha wanafunzi kuhusu maneno uliyoyataja mwanzoni mwa kipindi. Wakati mwingine wanafunzi watanyanyua mikono yao wakisikia ukisoma maneno hayo. Lakini ikitokea hawanyanyui mikono basi soma tena sentensi hizo taratibu, huku ukiwachokoza inapodi kwa kuwauliza, “kuna yeyote anasikia neno lolote kati ya yale tuliyotaja mwanzoni mwa kipindi?” Halafu utawaalika wanafunzi warudie neno hilo kwa sauti, na waombe wanaotaka kujitolea kueleza maana ya maneno hayo kadiri yalivyotumika kwenye sentensi. Itakuwa vizuri kama watayaandika maneno hayo kwenye madaftari yao kwa ajili ya kuwasaidia katika kujifunza kuandika.

2) Fikiri kwa sauti kuhusu maana za maneno. Soma sentensi ambayo ndani yake kuna neno lisilojulikana maana yake, na fikiri kwa sauti, ukionyesha kuwa unajaribu kufikiria maana yake kutegemea na muktadha (kwa kuangalia maeno mengine yaliyotumika pamoja na hilo neno).

3) Kujadiliana kuhusu Maneno. Waambie wanafunzi, kama hujawaambia bado, kuwa kujifunza maneno mapya kunawafanya wawe wazuri katika kufikiri. Waeleze kuwa utawafundisha baadhi ya maneno ambayo watayasikia kwenye matini utakayowasomea.

1. Tamka kwanza neno kwanza taratibu na kwa kusikika vizuri (lakini si taratibu sana). Tamka tena na waambie na wao warudie kulitamka neno hilo.
2. Eleza kwa kutumia maneno yako maana ya hilo neno.
3. Wape mfano wa muktadha wa matumizi ya hilo neno – mfano utokane na mambo ya kawaida waliyoyazoea kusikia.

4. Kama wanafunzi ni wakubwa kiasi cha kutosha, waulize wawili au watatu watoe mifano ya neno kama hilo kadiri ya uzoevu wao.
5. Waambie wanafunzi kusikiliza kama neno hilo limo kwenye matini ambayo utaisoma. Wanafunzi wakilisikia neno hilo, wanyoshe mikono yao.

Ramani ya kisemantiki (maswali ya kwenye mtandao)

Andika neno kwenye duara. Lama kuna wanafunzi darasani ambao hawajui vizuri Kiswahili, hakikisha unaonesha neno hilo katika lugha yao au zao. Pamoja na neno hilo andika “ni nini” kwenye duara linguine. Waambie wanafunzi wajibu swali hilo na uandike majibu yao pembeni kwenye duara la swali “ ni nini?” Andika sehemu nyingine “ikoje?” Waulize wanafunzi wajibu swali na andika majibu yao pembeni ya duara hili. Andika pia “ mifano yke ni ipi?” Waulize wanafunzi wajibu swali hilo, na andika majibu yao pembeni ya duara la“ mifano yake ni ipi?” Angalia mfano huu hapa:



Umbo mchemraba

Andaa umbo kubwa mchemraba kutokanayo na kadi za kuandikia, na katika kila sehemu ya umbo andika vifungu maneno vifuatavyo:

Elezea

Linganisha

Husisha

Chambua

Tumia

Unga mkono au pinga

Wanafunzi wawe na mada za kuandikia.

Waeleze wanafunzi kuwa wakati ukionyesha kila upande wa umbo, watatakiwa waandike kwa dakika mbili kadiri ya maelekezo yaliyopo.

Kama umbo linasema…

Elezea: watatakiwa kuelezea suala fulani au mada fulani katika hali ya uwazi…

Linganisha: watatakiwa kuandika jinsi kinavyofanana au kutofautiana na…

Husisha: watatakiwa kuandika jinsi kinavyowafanya wafikirie kuhusu uzoevu wao, masuala mengine au masomo mengine…

Chambua: wanafunzi watatakiwa kuandika kuhusu jinsi kilivyoundwa au kutengenezwa: jinsi watakavyochambua tatizo katika sehemu ndogo ndogo…

Tumia: Wanafunzi watatakiwa waeleze jinsi kinavyoweza kutumika, kinasababisha nini au madhara yake ni nini…

Unga mkono au pinga: Watatakiwa waseme kwa kuandika kama wanakiunga mkono au wanakipinga.

Onyesha kila upande wa umbo hilo lenye pande sita kwa dakika mbili. Baada ya kuonyesha sehemu zote sita za umbo, wape wanafunzi dakika nyingine mbili kuweka sawa kile walichoandika.
Kama huna umbo hilo, unaweza kuandika maneno kwenye ubao na kuonyesha kila moja unapoandika.

Mfano (Frayer Model)

Anglia jedwali hapa chini. Liandike ubaoni na waamboie wanafunzi waliandike kwenye ukurasa mzima wa madaftari yao. Andika neno la kujifunza katikati ya jedwali (kama

kuna wanafunzi wasiojua Kiswahili vizuro hakikisha unawatajia neno hilo katika lugha yao/zao). Kisha wambie wanafunzi wapendekeze maana ya neno hilo- wanafikiri lina maana gani- na andika maana hiyo kwenye kisandukucha juu upande wa kushoto. Kisha, waambie wanafunzi wapendekeze tabia zake-yaani, kitu kiwe na tabia hizo ili kiweze kuitwa kwa jina hilo. Kisha waambie wanafunzi watoe mfano. Mwisho, waambie wataje kitu kisicho mfano wake. Visivyo mfano ni vitu ambavyo vinafanana lakini vinatofautiana na mada inayozungumziwa. Wanakili kwenye madaftari yao maelezo kama yalivyo katika fomu iliyojazwa.

Mfano wa Frayer Model



Mbinu ya Saba : Uandishi

Kuandika ni sehemu muhimu sana ya kufundisha Lugha mama. Katika kitabu hiki cha mwongozo tunashughulika na kufundisha kuandika kama nyenzo ya kusaidia kufundisha kusoma. Wanafunzi wanapoandika maneno wakati huohuo wanajifunza kuyatamka na kutaja mwenedelezo wake inawasaidia sana kujifunza maumbo ya maneno. Wanapoandika ujumbe na wakati huohuo wanajaribu kuusoma katika matini inawafundisha sana kuhusu ufahamu wa kusoma.

Katika sehemu hii tutaangalia njia tatu za kufundisha kuandika. Kwanza ni kwa mwalimu kufanya kazi nyingi, kuwaonyesha wanafunzi jinsi maneno yanavyoandikwa. Pili, mwalimu kufanya kazi ndogo na badala yake wanafunzi wanafanya kazi zaidi kwa kumalizia sentensi ambazo mwalimu wao ametunga. Na ya tatu ni kuwafanya wanafunzi wafanye kazi zote peke yao: kutunga wenyewe ujumbe kuanzia mwanzo

Ujue kuwa utatakiwa kuwafundisha watoto zaidi juu ya uandishi kama stadi ya lugha zaidi ya ilivyowasilishwa hapa. Hapa tunashughulikia zaidi mbinu za uandishi ambazo zitasaidia zaidi katika kujifunza kusoma.

Maudhui ya sehemu hii ni:

- Uandishi wa kimawasiliano
- Vipande sentensi
- Mistari Mitano (Cinquains)
- Muundo wa Uandishi wa Kushawishi
- Warsha ya uandishi

Uandishi wa pamoja

- Uandishi wa pamoja ni njia ambayo mwalimu anaitumia kuwaonyesha wanafunzi jinsi maneno yanavyoweza kumegwa katika sehemu ndogo ndogo za sauti na herufi. Pia inasaidia kuwapa wanafunzi nafasi ya kuwa waandishi, kabla hawajaanza kuwa waandishi wa kazi zao wenyewe.
-
- Mwalimu anaanza kwa kuwashirikisha shairi au wimbo, au kujadili tukio fulani lenye msisimko kwa watoto, kama vile ilivyo katika somo la kujifunza kwa kutumia uzoefu wa lugha. Mwalimu anawaongoza watoto kuongelea tukio, au kuimba wimbo, au kusoma shairi.
-
- Halafu mwalimu huwataka wanafunzi wakubaliane kuhusu sentensi fupi wanazopenda kuziandika (inaweza kuwa sentensi kuhusu tukio fulani, au mstari wa shairi la wimbo). Mwalimu anawauliza watoto warudie kusoma sentensi mara kadhaa ili kila mmoja aweze kukumbuka maneno yaliyotumika wakati wa somo hili..
-
- Sasa mwalimu anawaalika wanafunzi wamsaidie kuandika sentensi, neno kwa neno. Mwalimu anataka kuwakumbusha wanafunzi kuhusu mpangilio wa maneno kwenye ukurasa. Kwahiyo anasema, “sasa tutaanza kuandika; tunaanzia wapi?”
- Watoto wanaonyesha upande wa juu wa kushoto wa ubao, na mwalimu anaweka chaki pale.
-
- “Tunaelekea wapi baada ya hapa?” Watoto wanaelekeza, nenda kulia, na baadaye nenda chini mstari mmoja halafu anza kushoto na kadhalika.
- “Sasa tutaandika neno la kwanza. Herufi ya kwanza katika neno la kwanza inatamkwaje ? Nani anaweza kutuambia herufi gani tuandike

hapa ? Mwalimu anaendelea kuwauliza watoto waendelee kutaja herufi wanazohitaji kwa kila sauti wanayotaja.

-
- Halafu wanarudia kusoma mstari mara kadhaa.

Uandishi wa Kimawasiliano

Uandishi wa kimawasiliano huwa na ufanisi zaidi kama vile kuandika maelezo kwa imla, isipokuwa hapa mwalimu na wanafunzi wanashirikiana kuandika kama ilivyokuwa kwenye njia ya uzoevu wa lugha kama tulivyojadili huko nyuma. Hapa tena tunaelezea hatua za kufuata:

1. Mwalimu na wanafunzi wanabadilishana uzoevu na kukubaliana kuhusu mada ya kuandikia. Mada inaweza kuwa kurudia kusimulia hadithi, shairi au wimbo, habari za kila siku, au wazo linalotokana na kinachosomwa siku hiyo darasani.
2. Wanafunzi wanatoa sentensi kuhusu mada husika. Mwalimu anawaambia wanafunzi warudie sentensi hizo mara nyingi, na ikiwezekana kuhesabu na maneno kwa lengo la kuwafanya wayashike vizuri kwenye vichwa vyao.
3. Mwalimu anawaambia wanafunzi wataje neno la kwanza, halafu analitamka neno hilo taratibu, na kuandika herufi zake.
4. Mwalimu anawaambia wataje neno linalofuata na kuwaambia wanafunzi waje mbele ubaoni kuandika neno lote au herufi kadhaa za neno hilo au herufi moja. Mwalimu anajaza herufi ambazo wanafunzi wameshindwa kumalizia. Ikiwa mwanafunzi anaandika herufi isiyo sahihi, mwalimu anafuta herufi hiyo na kumsaidia mwanafunzi kubaini jinsi inavyotamkwa na kuandika herufi sahihi.

5. Kila wakati neno litakapoongezwa, matini zima inasomwa tena na wanafunzi huku mwalimu akionyesha kwenye maneno.

Vipande Sentensi

Wanafunzi waliopata shida kuandika sentensi nzima wanaweza kumalizia sentensi ambazo umewaandikia ubaoni.

Sehemu za sentensi ambazo wanafunzi wanamalizia zinaitwa vyanzo vya sentensi na fremu za sentensi. Vyanzo vya Sentensi hutoa maneno machache ya mwanzo wa sentensi. Fremu za sentensi huacha nafasi za kujaza katikati ya sentensi ili wanafunzi wamalizie.

Kwa wanaoanza kujifunza kuandika, anza na vyanzo vya sentensi au fremu za sentensi kuhusu mambo yao binafsi. Wanafunzi wanajifunza kuandika majina yao kwanza, na mara nyingi huweza kuandika majina ya ukoo wao na marafiki.

Chanzo cha sentensi kwa anayejifunza kuandika kinaweza kuwa kama hivi,

Jina langu ni _____.

Majina ya wengine katika familia ni haya _____

Tunaishi _____.

Chanzo cha sentensi kwa wanafunzi wa kiwango cha juu zaidi chaweza kuwa,

Baadhi ya vitu ninavyopenda ni kama _____

_____.

Sipendi _____.

Lakini napenda sana _____.

Pia fremu ya sentensi cha kiwango cha juu chaweza kuwa,

*Napenda*_____

kwasababu _____

_____.

Sipendi _____

*kwasababu*_____

_____.

Fremu za Sentensi zinaweza kutumika mwisho wa kipindi kwa ajili ya kufupisha kile ambacho wanafunzi wamejifunza. Vinaweza kutumika pia baada ya wanafunzi kupewa hadithi ya kusoma au sehemu ya kitabu kwa lengo la kuwasaidia kufanya mapitio na kuhakikisha kile walichojifunza.

Kwa mfano, kama wamejifunza kuhusu miti, kwahiyo fremu ya sentensi inaweza kuwa,

Miti ni _____

_____

Baadhi ya aina za miti ni _____,

_____, _____,

na _____.

Baadhi ya miti _____,

Lakini mingine _____.

Mti ninaoupenda ni _____.

Tunatakiwa kuhifadhi miti kwasababu_____

_____.

Kadiri wanafunzi wanavyofanya zoezi la kumalizia vyanzo au fremu za sentensi, wanaweza kuinua mikono na kutaja majina wanayotaka kuyasoma. Wanapofanya hivyo wanaweza kuamua kwa namna kadhaa:

1) unaweza kuandika baadhi ya maneno hayo ubaoni na kuyaongeza kwenye ukuta wa maneno. Yanaweza kupangiliwa kwa makundi kama vile “Tunavyopenda na Tusivyopenda” au “Maneno katika Mti”.

2) Kama neno liko tayari kwenye ukuta wa maneno, unaweza kuwakumbusha wanafunzi kuwa wataliona hapo. Kama neno linafanana kimuundo na jingine lililopo tayari kwenye ukuta wa maneno basi unaweza kuwasaidia kulitafutia maana yake kwa kuangalia muundo wake.

3) Njia nyingine ni kumwomba mwanafunzi mmoja kulitamka neno na kutamka herufi zake (Tazama angalizo kwa mwalimu hapo chini).

Angalizo kwa mwalimu: Kubuni herufi
Wakati watoto wanapojifunza kutamka maneno, tunawataka wabuni herufi. Yaani, tunawataka wafanye kile wanachokijua kuhusu herufi na matamshi na wataje herufi za neno kadiri wanavyoweza.

Ni kweli kuwa mara nyingi wataandika kitu ambacho si sahihi. Lakini je, lina umuhimu wowote hilo?la
Wakiwa ni wanafunzi wanaoanza kujifunza, ni muhimu sana kwao kubuni kwasababu:

1) Inawafanya watafakari kuhusu jinsi herufi na sauti vinavyohusiana, na
2) Inakuonyesha vile wanavyojua na vile wasivyojua kuhusu jinsi maneno yanavyotamkwa. Tukijua nini wanahitaji kujua, ndipo tunapoweza kuwafundisha

Mfumo wa Uandishi wa Kushawishi

Mfumo huu utawasaidia wanafunzi kufafanua mawazo yao na kupangilia sababu zao katika hali ya kuweza kuwa na hoja au kauli za ushawishi.

2. Baada ya wanafunzi kupata fursa ya kutafakari, kusoma na kujadili mawazo yao, wapewe hamasa ya kukamilisha fremu ifuatayo (yaweza kuwa kila mmoja peke yake, katika jozi au kwenye kundi dogo):

Ni (tu) nafikiri kuwa: _____
Ni (tu) na sababu 3.
Sababu ya kwanza ni:
Ni (tu) nafikiri hivi kwasababu:
Ya pili ni:
Ni (tu) nafikiri hivi kwasababu:
Ya tatu ni:
Ni (tu) nafikiri hivi kwasababu:
Kwahiyo, Ni (tu) nafikiri kuwa tunatakiwa :

2. Kama muda utaruhusu, waambie wanafunzi wawashirikishe wenzao framu zao, ama kwa mwenzake au kwenye kikundi kingine.

Fremu ya Shairi: Mistari Mitano (cinquains)

Cinquains (neno la Kihispania, maana yake tano kwa maana ya mistari mitano ya shairi) ni njia nzuri nzuri sana ya kuwafanya wanafunzi waandike kwa ubunifu muhtasari wa kile wanachojua juu

ya walichosoma. ‘Mistari mitano’ hufuata mfumo huu ambao ni rahisi kabisa.

- Mstari wa kwanza una jina la mada.
- Mstari wa pili una maneno mawili ya kuelezea mada.
- Mstari wa tatu una maneno matatu ya kuonyesha kitendo
- Mstari wanne ni maneno manne ya kuelezea hisia, yanaweza kuandikwa katika vifungu maneno.
- Mstari wa tano ni neno moja ambalo ni kisawe cha neno lililotumika mstari wa kwanza.

Kwa mfano

Mwalimu
mbunifu, mwenye kufikiri
kupanga, kushirikisha, kuhamasisha
kuandaa kizazi kijacho
mwenye maono

Warsha ya Uandishi

Njia nyingine ya kuwahamasisha wanafunzi waweze kujua kujieleza kimaandishi ni kuandaa warsha ya uandishi. Warsha ya uandishi inaweza kuwa na hatua tatu tu:

1) **Kabla ya kuandika.** Hatua ya awali ni kuwahimiza wanafunzi kuchagua mada, kuijadili, kufikiri kitu gani wataandika kuhusu mada hiyo. Wale wadogo au ambao hawana uzoevu katika kuandika wanaanza na kuchora kwenye madaftari yao, na kuongeza maneno wanayoweza. Wanafunzi wakubwa watabungua bongo kidogo kwa kutafuta maneno ya kuandika. Watayaorodhesha mawazo yao. Baadhi ya wanafunzi wanachora picha kama mwongozo wa kupata maana za maneno, yaani ramani ya kisemantiki. Ramani ya

kisemantiki inakuwa na mada kuu kwenye mduara wa katikati, na mawazo mengine yenye kuhusiana na mada kuu huwekwa pembeni kuizunguka mada kuu:



Baada ya kubungua bongo kuhusu orodha ya mawazo muhimu, au mwongozo wa kisemantiki, wanafunzi wanaweza kujadili wawili wawili kwa lengo la kupata mawazo zaidi kuhusu mada yao. Lakini isiwe sana: unatakiwa ubakize kitu fulani kwa ajili yao ili waweze kuandika.

2) **Kuandika rasimu.** Baada ya wanafunzi kupata mawazo fulani kuhusiana na kile watakachoandika, wanaweza kuandika muswada wa mawazo yao. Kwa wale wanaoanza kujifunza kuandika, hii inaweza kuwa uandishi wa maelezo mafupi, au ufafanuzi chini ya picha. (Wakumbushe kuacha nafasi ya kuandika maelezo ya picha kwenye ukurasa husika). Wengine wanaweza kuruka mstari kwenye madaftari yao wakati wa kuandika ili kuacha nafasi ya kuongeza mawazo mapya hapo baadaye.

3) **Kushirikishana.** Waandishi wote hupenda kushirikisha kile walichoandika. Wanafunzi wanaweza kuombwa wawashirikishe wenzao kile walichoandika, inaweza kuwa mwenzake aliyekaa naye, au kikundoi kidogo. Wanafunzi wawili au watatu wanaweza kuitwa mbele ya darasa na kuwashirikisha wenzao kile walichoandika. Waite waandishi wakiwa wameandika kitu fulani wanachotaka kuwashirikisha wenzao. Jitahidi kuwafundisha wengine kuwa wasikilizaji wazuri. Unaweza kuwakumbusha umuhimu wa kupongeza na kuuliza swali.

Angalizo kwa mwalimu: *Mwalimu ndiye anayeanza*!
Hii inamaanisha nini?
Baadhi ya watu wanalinganisha kufundisha kuandika kuwa sawa na kufundisha kutengeza vyungu, au kufuma vikapu. Unafundisha kutengeneza vyungu na kufuma vikapu kwa kuwaonyesha wanafunzi kwa kutumia kazi yako kama mfano. Unaweza kuwafundisha wanafunzi kusoma kwa njia hiyo pia.

Unapowaanzisha mchakato wa kuandika, onyesha hatua hizo ubaoni. Fikiria kuhusu mada na chora picha kushusiana na hiyo mada. Andika mawazo yako. Halafu washirikishe wengine mawazo hayo. Wanafunzi watapenda unavyoafanya. Na watajua cha kufanya.